
Sciamanna Mario sx



# MASHAHIDI WANNE WA YESU KRISTU KATIKA CONGO

Pitcha katika ukurasa ya mbele: kisima cha ubatizo pa Fizi (1970) iliojengwa pa nafasi ya uuaji ya padri Didonè na abbé Joubert. Ni kusema: Damu ya Wafiadini ni mbegu ya wakristu wapya.

# SEHEMU YA KWANZA: hali ya Congo mwaka 1964

## Kipindi cha 1: Congo katika zoruba kiisha uhuru

Congo, kiisha kupata uhuru (1960) iliingia katika zoruba na magumu ya kila aina: vita ya waasi (rebelles) iliwaka katika pande zote. Waasi walikuwa wote wakongomani, lakini mawazo na nia zao ziliongozwa na nchi za kigeni: Russia, China, America, Ubeleji, Afrique du Sud. Nia ya nchi za kigeni ilikuwa kuingia katika Congo, kutawala na kuiba mali yanayofichika katika udongo: zahabu, coltan, shaba na alimasi. Fujo na vita vinasaidia wizi wa Congo: moto wa vita ulitoka kwa nchi ya kigeni. Wageni walioleta vita walileta pia mawazo mapya "Communisme athée" iliyo adui ya dini ya kikristu; ndiyo sababu Maaskofu, Mapadri Misionari, Mapadri Wakongomani, Masera misionari na wakongomani, hata Waseminarista, waliteswa na kuuawa.

Siku 18 Mai 1964 Gaston Soumialot, mkongomani, ni mmoja kati ya waongozi wa Waasi Wamulele; anaanza vita ya waasi mjini Bukavu (Kivu).

Pierre Mulele anaanza vita ya waasi katika Bandundu siku 2.8.1963. Waasi wake waliitwa simba "lions".

Pierre Mulele alizaliwa katika Bandundu siku 11.7.1929; alikuwa msaidizi wa Lumumba, na mwaka 1960 "Ministre de l'éducation nationale". Wakati Lumumba alifungwa, Mulele alikimbia katika nchi ya China, na pale alishibishwa na mawazo na nia ya "communisme-maoiste". Waasi wa Mulele (Mulelistes) walianza vita katika nafasi mingi ya Congo. Hata katika Congo kulikuwa sababu ya kupindua mambo, na kuanza vita ya upinduzi. Mulele alisikia malalamiko bila matumaini ya Wakongomani walioona ya kama nyuma ya kutangazwa uhuru, umaskini na mambo mabaya mengi yaendelea, kama vile mbele

ya uhuru. Kwa kujisaidia na kujilinda, tena kwa kuogopesha watu, Wamulele walifuata mambo ya ulozi na ya ufumu. Mawazo makubwa ya kuongoza Wamulele watende kwa ujeuri ni “communisme-maoiste” ya China. Kubomoa Eklezya katolika ilikuwa nia yao, kwa sababu Wamisionari Weupe ao Weusi, wanafundisha uhuru mbalimbali na uhuru ya “communistes”, tena uhuru wa kweli unazuia matendo yao.

Stanleyville (Kisangani) siku 4.8.1964 inatangazwa kama vile “Capitale de la République Populaire du Congo”, na “Armée populaire de libération”, na Quartier général. Wamulele wanaongozwa na Wakongomani waliojifunza “communisme” katika Russia ao China; ndiyo sababu waliwafuata na kuwatesa Wamisionari, mapadri ao mafrera wanaotoka Ulaya, tena mapadri, watawa na mabikira wakongomani. Pamoja na wakongomani wanaoongoza wamulele walikuwa pia wageni; wamoja wanatoka Russia, China na Cuba.

Wasimba walikuwa tayari kutoa maisha yao, wakisukumwa na “matérialisme athée, revolutionnaire et antireligieux, marxiste-léniniste africanisé” kwa kobomoa Eklezya katolika. Husema Lumumba ni mkubwa kuliko Yesu Kristu; huyu ni Masya wa wazungu, lakini Lumumba ni Masya wa weusi. Ndiyo maana Mapadri, Wafrera, Wabikira waotoka Ulaya, na Mapadri, wafrera na mabikira wakongomani wanafuatwa na kuteswa sababu ni watu wanaoungana na Kristu na Eklezya, na kazi yao ni kumshuhudia Kristu na kutangaza Enjili yake.

Ndiyo « odium fidei »: kuchukia imani ya kikristu.

Alama ngine ya kama Wamulele waliwaua watu, si sababu ya rangi (razisme) au sababu ya ukabila (tribalisme) ila sababu ya kuchukia imani ya kikristu « odium fidei »: kati ya mashahidi tunakuta Mapadri, Masera, Waseminarista na walaiki Wakongomani. Ushuhuda kwa Yesu Kristu ulikusanyisha pamoja Wamisionari wanaotoka mbali na Wakongomani: imani moja, mapendo mamoja kwa Yesu Kristu, ushuhuda mmoja.

## Zoruba inaanza katika Misioni ya Kibanga

Kiisha miaka tano katika Seminario ya Mungombe, mwaka 1964 abbé Albert Joubert alitumwa Kibanga, katika Ubwari pamoja na mwenzake Thomas Maliyabwana. Ukomo wao: kufungua tena Misioni ya Kibanga iliyoundwa mwaka 1883 na kufungwa mwaka 1893. Askofu wa Uvira, Catarzi, na Askofu wa Kasongo, Mala, walipendelea sana Kibanga, katika Ubwari, sababu asili ya Askofu Mala ni Ubwari na yeye ni Mbwari.

Mapadri hawa, wote wawili wakongomani, wanapata magumu mengi na Wamulele, hata hatari ya kufa. Albert, akiona hatari ya kufa, angeweza kuvuka Tanganika na kukimbia Bujumbura, lakini alibakia Kibanga, pamoja na kondoo za Mungu. Siku 10.9.1964 Albert na Thomas wanakamatwa na kupelekwa Fizi; walipoacha Kibanga, wakristu walilia machozi, waliomba baraka ya mapadri mbele ya kuachana. Albert na Thomas wanafungwa gerezani, wanapigwa, kiisha wanafunguliwa, kisha juma mbili ya mateso. Albert anabakia Fizi kwa kumsaidia Padri Giovanni Didonè; alikataa kurudia Kibanga, kwani wakristu wakasambazwa; Kibanga ilikuwa mji wa lazima kwa Wamulele wanaosaidiwa na 144 waaskari wa Cuba. Mwaka 1965 alifika Kibanga Che Guevara, mkubwa wa waaskari wa kuajirihwa (mercénaires) wa Cuba: aliacha Congo ule ule mwaka mwezi wa kenda, sababu alikataa namna ya kufanya upinduzi ya Wakongomani

Katika misioni ya Fizi na Baraka, wakati huo, wanatumika Mapadri Carrara na Didonè pamoja na frera Faccin; wanasaidiana katika Misioni mbili.

Wakati Albert anafika Fizi, anakuta Padri Didonè peke yake, kwa sababu P. Carrara alikuwa Baraka pamoja na frera Faccin.

## Zoruba inaanza katika Misioni ya Fizi

Albert na Maliyabwana walifungwa katika gereza ya Fizi muda wa siku kumi, tangu 10.9.1964 mpaka siku 20.9.1964. Albert

alitumika Fizi pamoja na Didonè siku 69, tangu 20.9.1964 mpaka siku ya kutoa uzima wake kwa ajili ya Yesu Kristu: 28.11.1964.

Padri Carrara alifurahi sana na matunda ya kazi ya kitume katika Misioni ya Fizi. Padri Didonè alijitolea kwa kuadibisha na kufundisha wakatekista. Didonè na Albert, wakiishi pamoja katika Misioni ya Fizi, wanaona kama uzulumu na hatari ya kufa kwao inakaribia. Siku 9.11.1964, Didonè anamwandikia Raphael Pupu, mkatekista wa Muzinga, karibu na Ngandja; barua hii ni namna ya kuagana, sababu kifo cha mapadri ni karibu.

> "Tubakie wima. Tusiwaze kama mapadri watarudia kwao. Mjue wazi ya kama mapadri, pahali pa kurudia kwao, wanapenda zaidi kufa katika Misioni".

Kufa kuliko kuacha peke yao kondoo wa Mungu: ndiyo nia ya Didonè. Albert alikuwa pamoja naye, hapo nia ya Didonè ilikuwa pia nia ya Albert: kubakia ndiyo, kukimbia hapana. Albert hakusema kitu, hakuandika barua, lakini hakukimbia, alibakia pamoja na Didonè, kwa kulinda wakristu na wakaaji wote.

## Zoruba inaanza katika Misioni ya Baraka

Padri Carrara na frera Faccin wanatumika pamoja pa Baraka. Wamulele wanashambulia Misioni: mwezi wa tano 1964 wanakamata gari, mtumbwi na kinga ya Misioni. Wakati wakristu wanapiga kengele kwa sala, chuki na hamu ya kuua ya Wamulele zinaongezeka. Frera Faccin anaandika barua mingi kwa wazazi, akiwafasiria hatari, na kuomba msaada wa sala.

> "Tupo hapa, tunangoja tu. Kutatukia nini, Mungu peke yake anajua. Tunaomba tu mtuombee mbele ya Bikira Maria, mama yetu wa mbingu… Msilie juu yetu: mtukubumbuke katika sala zenu, ili Mungu atukuzwe na atupatie sisi wote nguvu ya kushuhudia sifa yake" (Baraka 25.5.1964).

Padri Luigi Carrara aliisha acha Fizi, kwa kubakia Baraka, pamoja na Frera Faccin. Padri Mkongomani Maliyabwana, mgonjwa, kutoka Fizi anarudia Kibanga siku 20.9.1964, na nia ya kufika Burundi kwa kutunzwa ugonjwa wake wa sukari.

Wamulele wanawaza (na uwongo) na wanashtaki Mapadri kama wana "Radio-émetteur (phonie)", na chombo hiki wanaongea na "Armée Nationale" kwa kuwaonyesha nafasi ya Wamulele. Hata wakristu, sababu ya woga wa Wamulele, wanawaza vile na wanaanza kuishi mbali na Mapadri. Wabembe wamoja wanaingia katika jeshi la Wamulele.

Katika Misioni ya Baraka, wakati frera Faccin anaendelesha majengo ya kanisa na nyumba, Padri Luigi Carrara anapitisha mchana mzima kanisani kwa kusali, akipiga magoti. Usiku Carrara na Faccin wanaogopa kulala katika Misioni; jamaa moja ya shirika Matata inawapokea nyumbani wapate kulala na amani. Ulikuwa mwanzo wa mwezi wa kenda; katika Ubembe Mapadri peke yao wanabakia; Waarabu wachuruzi waliisha kukimbia.

Kama Wamulele wanashindwa na kuuawa, wanasema: kosa ni la Mapadri sababu ya "Radio" yao.

## Uvira: Mapadri Xaveriano, mateka ya Wamulele

Siku 15 Mai 1964 waasi wamulele walikamata Uvira. Wabeleji na watu wengine wa Ulaya walikimbia na walirudia kwao. Walibakia Uvira waxaveriano 12, masera 12 na walaiki wamoja. Hawa wote walifungwa katika nyumba ya Askofu kama vile mateka; walipata magumu na mateso mengi: walipigwa makofi, kutembea miguu kanya, kupigwa kichwani na vyupa na kutoka damu; woga wa ajabu. Waasi walikuwa na chuki na asira kubwa kwa dini na Eklezya katolika; katika mawazo na nia zao walikuwa wakiongozwa na kundi ya "chinois" waliokaa Bujumbura: mawazo na nia za "Communistes Chinois" ziliongoza Wamulele.

Waxaveriano waliofungwa Uvira, siku moja, walipokea kopo ya nyama inayotoka China. Mwanzo wa uzulumu Askofu Catarzi aliwapatia wafungwa wote, kwa jina la Mungu, mandoleo ya zambi kwa jumla, na aliwaambia kitu gani kitaweza kuwatukia, sababu ya kuwa wamisionari. Kwa mara tatu wafungwa walipelekwa kwa chumba cha hukumu, walipigwa, walilazimishwa kukaa chini juu ya vpande vya sahani, na kuogofya kufa. Siku moja, kiisha hukumu ya wongo, walifungwa katika kalabozo; waliwatosha wawili wawili kwa kuwaua;

walikamata Tonino Manzotti, walimpeleka katika nyumba ya Mzungu mmoja, kiisha walisikilizisha wafungwa wanaobakia ndani mlio wa bunduki kwa kusema kama kweli walipigwa masasi. P. Manzotti hakuuawa. Siku moja Askofu Catarzi alimwuliza Mlele anayesema kama ni mkristu, namna gani anatenda vile; Mulele alimjibu, akimpiga Askofu usoni na tako la bunduki yake. Mateso mengine, kusukuma ngungulu ya peteroli.

Katika hali ya uchungu na mateso, wamoja walilalamika na kusema: “Ee Bwana, tafazali kufa; uniache, niko mkristu”. Bikira mmoja analia machozi.

Usiku moja ulioweza kuwa wa mwisho, mapadri, masera na walaiki wanasali kwa kujitayarisha; asubui na mapema wanafuata Misa na wanakomunika: ndio mkate wa safari ya kurudia kwa Mungu.

Siku 27 Augusti, saa 8h30 avions mbili T 28 zinatoka Bukavu kwa kupigana na Wamulele na kuwafungulia wafungwa. Hasira ya Wamulele inazidisha hatari ya kufa ya wafungwa.

Kiisha miezi tano ya mateso, siku 07.X.1964 “Parachutistes belges” pamoja na P. Angelo Pansa wanawapatia waliofungwa wa Uvira kama mateka, ukombozi na uhuru.

Wakati huo Mapadri wa Kiringe, Kamituga na wa Misioni zingine wanaomba kwa mkubwa wa “Xavériens” ruhusa ya kubakia, sababu hawapendi kukimbia, hawapendi kuacha kundi ya Mungu isambalane. Askofu Catarzi, katika barua ya 10.7.1964 anahakikisha: “Mapadri na wafrera, japo hatari ni kubwa, wanabakia katika Misioni yao kwa kulinda misioni. Wanakataa kuacha kundi ya Mungu. Tunapenda kubakia mpaka mwisho”.


Lakini Mapadri wa Mulenge, mji mkubwa wa waasi, walipashwa kukimbia mwanzo wa mwezi wa tano 1964: walitembea na miguu Kilometri 100 katika milima, kwa kupata amani kidogo.

## Bukavu: vita na Wamulele

Siku 17 Februari 1961, pa Bukavu aliuawa Padri Réné de Vos (Père Blanc), Padri Mkubwa ya parokya ya Kadutu.

Bukavu, mwezi wa nane 1964 watu wamoja wa Ulaya, kiisha kupoteza mali yao yote sababu ya vita, wanafanya kundi moja

kwa kusaidia “Armée Nationale”. Kiisha mapambano mawili na Wamulele, hawa wanaanza kushindwa: waasi wengi walikufa pa Bukavu. Mobutu “Général de l’Armée” pamoja na “Colonnel” Mulamba, walishinda na waliua Wamulele wengi pa Kamanyola. Na “avions bombardiers” T28 na B22 “Armée nationale” iliwasambaza na kuwaua Wamulele. Asira kali na hamu ya kujilipiza kisasi zinaongeza ukali na ujeuri wa Wamulele: hatari kubwa kwa Wamisionari.



17.2.1961 : Bukavu : Père Blanc. P. Réné De Vos
1.1.1962 : Kongolo : 20 Spiritains
22.1.64 : Kilembe : 3 Oblats
26.6.64 : Nakiiza(Uvira) : Ettinger Edoardo. Provincial Maristes.
22.7.64 : Kindu : Lucien Vandamme, frère Mariste.
7.8.64 : Kabondo (Kisangani) : Abbé Munyororo.
11.8.64 : Lubuye (Kalemie) : 2 Pères Blancs.
7.9.64 : Bonginda : 1 frère Mill-Hill et 3 Soeurs.
23.X.64 : Tchumbe : Lambert Jansen, passioniste.
8.11.64 : Basankusu : 1 Père MiIl-Hill.
24.11.64: Paulis : P.Armani Remo, combonien. 11 Mission. protest.
25.11.64 : Kisangani : 10 Pretres S.Cœur, 15 soeurs.
25.11.64 : Paulis : 4 Dominicains.
26.11.64 : Mambasa(Pygmées) : 4 Petits frères de Jésus.
26.11.64 : Watsa : 6 Dominicains, 9 Sœurs de Namur.
26.11.64: Wamba: L'Evèque Wittenbols, 7 pretres S.Cœur.
27.11.64: Kisangan: 3 Mill Hill.
27.11.64 : Mahagi : 6 Pères Blancs, 4 Soeurs de Marie.
27.11.64 : Bafwasende : 7 Pretres du S. Cœur.
28.11.64: Fizi-Baraka: P. Didonè, P. Carrara, Fr. Faccin, Ab. Joubert.
1.12.64 : Paulis (Wamba) : Bse Soeur Anwarite Nengapeta.
1.12.64 : Bunia : 3 Pères Blancs.
1.12.64 : Rungu : 3 Dominicains et 3 Comboniens
27.12.64 : Birindi : Bx P. Spoto Francesco, Serviteurs pauv.
22.2.65 : Mahagi : Abbé Gonzalve Nsandi et un grand Sem.
6.6.65 : Idiofa : Abbé Lamkwan, 1 Sèm. 2 élèves.
30.5.65 : Buta: 3 Pères Capucins, 20 Pères Croisés, 7 frères St Gabr.

**Nombre de martyrs par Congrégation**

Soeurs missionnaires et congolaises: 32
Sacré Cœur: 28
Spiritains: 20
Pères Croisés: 20
Dominicains: 13
Pères Blancs: 12
Frères de Saint Gabriel: 7

Petits Frères de Jésus: 4
Comboniens: 4
Xavériens: 3
Capucins: 3
Mill-Hill: 3
Frères Maristes: 2
Passioniste: 1
Mission Protestante: 10 blancs
Abbés cong.: 4
Seminaristes cong: 2
Jeunes cong: 3

TOTAL: 135 HOMMES + 32 SŒURS
Total Général: 167 martyrs.
Nota bene: Agence DIA du 18 Avril 1966 donne des statistiques plus complètes:
182 religieux (114 pretres, 29 frères, 38 sœurs); 1 Séminariste



Église de Baraka (Photo de 1970).
Frera Faccin na padri Carrara waliuawa mbele ya kanisa
(cf. étoile rouge).

## Kifo cha Askofu Wittebols na cha misionari wenzake

Tupo katika Diosezi ya Wamba; Askofu wa Diosezi ni Wittebols, misionari wa “Sacré Cœur”; wenye kumsaidia ni wenzake Misionari wa “Sacré Cœur” pia.

**17 Novemba**

Hasira na chuki ya Wasimba zinaongezeka. Wakati wa usiku P. Ch. Bellinckx anafungula dirisha ya chumba chake; simba mmoja, anapita katika barabara, anaona. Kesho yake, asubui “lieutenant” na askari sita wanakuja kwetu, kwa Misioni; anatukusanyisha katika kiwanja cha ndani; wanamshtaki P.Bellinckx kama alifanya kosa kubwa alipofungua dirisha kwa nia ya kukimbia: anastahili kifo; Padri alifungwa, hakuuawa, lakini walimpatia malipizi makubwa: kutosha nguo na kulala tumbo chini: ni usumbufu wa “chinois” ulioletwa na Simba katika Congo; wanafunga na kamba mikono ya Padri nyuma ya mabega; Padri analalamika; kiisha wanafunga na kamba miguu na kuiunganisha na mikono; kifua tu kinagusa udongo; Padri anabakia vile dakika kumi na tano. Sisi tulikuwa pale, na wofu kubwa sana, bila kuweza kufanya kitu isipokuwa kusali; walipomfungua Padri alikuwa kama vile mwenye kupooza, udongoni; tunamsimamisha, tunamtia katika kitanda; pole pole alianza kutukutika. Kalvario yetu inaanza.

**24 Novemba**

Siku 24 Novemba “Parachutistes Belges” walikomboa Kisangani. Mgreki mmoja alitupasha ile habari kwa siri. Mangaribi ya ile siku jehanama ilitomboka. Tulikuwa Mapadri watano na Wafrera wawili pamoja na Askofu Akina Wittebols; tulikuwa tukisali sala ya mangaribi. Kwa rafla mlango ulifunguka na fujo kababmbi. Kundi ya Wasimba iliturukia na bunduki mikononi, kama vile kwa kutupiga kifuani; walitupiga na miguu yao na tako la bunduki, wakitusukuma pembeni. Mwisho walitusukuma mpaka Misioni yetu, karibu na nyumba ya Masera na nyumba ya Askofu. Katika Misioni tunakuta Mapadri wengine; wao pia walipigwa mpaka damu. Walitulazimisha

kutosha vyatu na stokin (chaussettes) na kuwapatia mataratala yetu na saa. Padri mkubwa alilazimishwa kufungua sanduku la feza; walikamata franka yote. Walituweka kwa mstari katika baraza ya ndani; nyuma yetu, katika mstari wa pili waliweka wazungu wengine, walimaji wa kahawa; mmoja kati yao alipata wazimu, aliruka katika baraza la nje, akijaribu kukimbia.

Wasimba walimfuata, walimshika na walimrudisha katika baraza, walimchoma na mikuki yao, alikufa mbele ya macho yetu. Walitupeleka kwa gereza, iliyo mbali na Misioni 500 metri, katika mstari, miguu kanya, na mwendo wa haraka; kwa jumla tulikuwa 34. Katika kichwa ya mandamano anajaribu kuenda haraka Askofu Wittebols; bila luneti, mgonjwa wa macho, maskini Askofu anaanguka kila hatua, katika giza ya usiku; halafu wanampiga na ngumi usoni, wanampiga kichwani, na tako la bunduki wanampiga mabegani. Kwa mwendo wote, Wasimba wanakimbia ngambo na ngambo ya mstari, wanatupiga kwa kuharakikisha kutembea. Hakuna namna ya kuepuka mapigo; hasa Askofu aliteswa sana, simba mmoja anamfuata na anaendelea kumpiga bila kupunzika. Tunafika kwa gereza, bila nguvu hata moja, wazaifu karibu kufa. Katika kiwanja ya ndani walitulazimisha kujilaza chini, tumbo udongoni; wasimba na vyatu vyao vya askari wanatembea juu ya miili yetu; ole yule anayejaribu kusimama, anakanyagwa na kurudishwa chini; kwa kumaliza, wasimba wanatosha mikaba yao na wanatupiga kama nyama ya kazi; mwenye analia na kulalamika anakamata azabu mara mbili. Sauti moja ilisikilizwa "Kwa leo inatosha". Mlango moja wazi unapeleka ndani ya gereza; kwa kuepuka mapigo tunaenda mbio, kiisha, sababu ya haraka na giza tunaporomoka, mmoja juu ya mwenzake, katika shimu iliyokuwa mbele ya mlango. Wakiona vile Wasimba walinzi waliokuwa karibu na moto, walitupa juu yetu miti yenye kuwaka moto; wengi kati yetu waliumiwa na moto. Mwisho tunakutana katika chumba moja bila madirisha, ndio mgogoro.

Katika giza, tunakaa chini karibu na ukuta; tunasikia mateso kali sababu ya vidonda vinavyotosha damu. Usiku, bila kulala, ulionekana bila mwisho. P.Vandemoere alianza kutapika mingi.

Askofu alikuwa na mateso kali, alihangaika sana: kusimama, kutembea kidogo, kukaa chini tena: usiku mzima vilevile. Asubui, kwa mwangaza wa mchana tunaona mavazi yetu yanayochafuka na damu. Sisi wote tunapoteza damu; sehemu ya mbele ya kanzu ya Askofu inafunikwa na taka kubwa ya damu. Muchana ulipita na huzuni na mahangaiko ya ajabu. Upande wa 17h tunasikia sauti "Wote katika kiwanja ya ndani". Colonnel "mmoja alitugabula katika makundi matatu: Waamerikani, Wabeleji na wasio Wabeleji. Katika kundi ya Waamericani wawili walikuwa Misionari Waprotestanti. Waamericani wote walitupwa chini; simba moja anawakanyaga na miguu yake; wanatupwa ndani ya gari kama vile vitu vya kutupa; wanawapeleka kwa mtoni na kuwatupa ndani ya maji.

Zamu ya Wabeleji inakuja; Askofu Wittebols anashtakiwa kama anaficha "Radio émetteur" kwa kuwaita Waamericani waje Wamba; walimwondosha msalaba wa kifua wa kiaskofu, walimpatia P. Beutener na kusema kwamba, tangu leo, yeye ni Askofu wa Wamba. Kiisha walimwambia Askofu "Uite sasa Waamericani na radio yako; walimlazimisha kulalamika (bila radio) katika luga ya Flammans "Nafugwa hapa Wamba, mje na avions zenu kunikomboa". Kiisha Kapita moja anakuja na anatuambia: "Mrudie katika Misioni, lakini msifanye politique". Upande wa 19h milango ya gereza inafunguliwa mbele yetu. Mapadri wawili wanamsaidia Askofu kutembea. Tunanawa, tunakula kidogo na tunaenda kulala; saa moja kiisha usiku kati Wasimba wanarudia, wanaangalia tena "documents" kwa kutambua Wabeleji; Wabeleji wanarudishwa tena katika gereza: ni mara ya mwisho ya kuona Askofu wetu na wandugu wetu Wamisionari 7 Wabeleji.

**26 Novemba**

Asubui ya 26 Novemba ilipita bila magumu mengine, lakini na hali ya huzuni. Walipeleka wapi Askofu na wandugu wetu Wabeleji saba? Pa 13h tunasikia ngurumu ya bunduki ya kupiga masasi. Kiisha kidogo Kapita mmoja alifika kwa Misioni kwa kuchungua vizuri nyumba ya Askofu. Nilimwuliza juu ya shindo la bunduki la mbele kidogo. Kwanza hakupenda kujibu, kiisha alisema "Labda mtu aliuawa". Kesho yake, asubui, 27 Novemba,

anafika mtu anayejitaja “Officier Judiciaire” kwa kuchungua vizuri makao ya Askofu, chumba cha kulala na chumba cha kupokea watu; alifunga milango na funguo, kiisha anaiweka katika mfuko; kiisha anaandika na chaki katika mlango wa kuingia “Alikufa”. Alifanya vile vile katika vyumba vya wandugu wetu 7 na katika vyumba vya walimaji 6 Wabeleji. Kumbe Wamisionari wenzetu na walimaji waliuawa.

Mangaribi mwanafunzi mmoja wa Kisangani alifika kuniona; alinifasiria namna gani wenzetu waliuawa. Asubui na mapema, siku 27 Novemba, Wasimba walitembea katika mji wote kwa kualika watu wafike kuona namna gani wazungu watauawa; wote wanapashwa kufika na mikuki na visu. Wakati watu wote waliisha kukusanyika, walitosha kwa gereza wale wafungwa 24; walilazimisha kuvaa tu suruali fupi na yenye kukamatilia mwili, kujilaza katika majani karibu na ukuta. Wamulele walipiga masasi katika kichwa ao mabegani ya wafungwa, nao walikufa. “Colonnel” alijipatia sifa ya kuua Askofu Wittebols, mbele ya wengine wote. Watu walilazimishwa kukatakata maiti vipande vipande, na mikuki na visu. Mlinzi wa Misioni, mtumishi mwaminfu, alilazimishwa kukata na shoka mguu mmoja wa Askofu, yeye aliyekuwa na heshima kubwa kwa Askofu.

Yaliyobakia ya maiti waliyatia ndani ya gari na kuyatupa katika Wamba, kijito kinachopita karibu na Misioni. Maji ya kijito yalikuwa madogo, sababu ya kipwa: maiti yalioza chini ya jua kali ya Congo. Siku mbili nyuma wasimba waliua wabeleji wengine wanne, kati yao waganga wawili: Lambert na Swerts; Swert aliongoza Hopitali ya wakoma wa Pawa, karibu na Wamba.

Kati ya Wamisionari wa “Sacré Cœur” wasio Wabeleji, wengi walikuwa wa Olanda. Mwisho Wamisionari wanane walipata uhuru: frera moja wa Yugoslavia, watatu wa Luxemburgo, mmoja wa France, mmoja wa Suisse, mmoja “wallon”. Kiisha wengine wote walipata uhuru.Kiisha Wamisionari walirudishwa katika gereza. Wakubwa walibishana kati yao juu ya hali ya wafungwa. “Inafaa kuwaua wote”, ”Hatuna haki ya kuwaua”. Kiisha “Commandant” wa Wamba alisema “Siwezi kuwaua; sikupata ruhusa ya Général”. Mwisho wamisionari wa ”Sacré

Cœur" waliobakia, walikombolewa na waaskari wa kuajirishwa (Mercénaires).

Wamisionari wengi, wa nchi mbalimbali; mapadri, wafrera na masera wacongomani waliuawa katika Congo mwaka 1964. Tunaweza kukumbuka "Pères Blancs" wa Lubuye (karibu na Kalemie) na hasa uchinjaji wa Kisangani.

## Njia ya msalaba ya "Pères Blancs" mjini Lubuye

Siku 11 Augusti 1964, mjini Lubye, pa saa kumi na mbili (6h du matin), Wamulele wanafika kwa Misioni, wanaamuru Mapadri wawafuate mpaka "Quartier Général de l'Armée populaire de la révolution" Mapadri Stove na Lenaers walipashwa kukata Misa katikati. Masera waliweza kubakia. Mapadri walizarauliwa: kutosha luneti, kuimba na tawi la mhogo mikononi, kupita katika soko na miguu kanya, kupigwa mabegani. Waliwaogopesha wakisema kama wote watakufa. Mapadri waliungama wao kwa wao. Mapadri wanaenda na miguu; kijana mmoja na bunduki anawafuata nyuma, karibu. Padri Stove aliangalia nyuma: pale pale alipigwa masasi, alikufa bila kusema kitu. Padri Lenaers vile vile aliangalia nyuma kwa kujua inatukia nini, aliuawa. Padri Van Audenaerde alilazimishwa kutoka kwa gari; alivuka maiti ya wandugu waliokufa, alianza kukimbia na kulia: "Naenda mbinguni. Mungu atashinda".

Walimpiga masasi mbili, lakini Padri hakufa, alipoteza tu damu mingi; aliingia tena katika gari na walimwambia asichafue na damu yake godoro "matelas" waliyoiba. Wandugu wawili waliouawa, kesho yake walizikwa, katika shamba la wafu, karibu na Kristu Mfalme. Misionari 18 na Mapadri wakongomani 6 walipelekwa kwa kinguvu Kalemie, kutoka Sola, Bulula, Makutano na Nyunzu; walifungwa muda wa siku 8, walikuwa karibu buchi, ;walipigwa; muda wa juma tatu waliishi pamoja na wamulele, wakikula chakula chao, hasa maharagi. Masera wa Ulaya na wa Congo waliwaacha bila kuwasumbua. Tupo katika mwezi wa nane 1964.

## Uuaji wa Kisangani (22-28 Novemba 1964)

Frera mmoja Mkongomani Richard Mabanza aliandika matukio yote ya Kisangani.

Siku 22 Novemba 1964, katika nyumba ya "Pères du Sacré Cœur, " pa Kisangani walikusanyika, kwa amri ya Wamulele: Wamisionari 74 (Mapadri, Wafrera, Masera) na jamaa moja ya Waprotestanti. Mapadri waliotoka Ubuntu na kufika Kisangani kwa gari ya moshi, katika "rive gauche" ya mto Congo, walipelekwa bila kukawia ngambo ya "rive droite". Walibakia katika Misioni, ngambo ya kushoto "rive gauche" Wamisionari wawili: Padri Bosh, frera Damiano na wafrera wacongomani watatu: Jean Marie, Cyprien na Richard. Usiku kati ya ile siku ya Mungu Wamulele walifika kuamsha Padri na Wafrera 4, ili wapokee Masera wanaotoka Ubuntu. Wamulele walipeleka Padri Bosh na Frera Damiano katika gereza ya "rive gauche".

Siku ya pili, asubui, 24 Novemba walifika katika "rive droite" "Paracadutistes belges" na avions ya Waamerikani; waliokoa watu wa Ulaya, mateka wa Wamulele, na kuwapeleka kwao, kwa njia ya Kinshasa. Wamulele walikasirika sana na waliwaua watu 28 wa Ulaya. Saa tano ya asubui ya ile siku, Wamulele walirudia katika misioni ya "rive gauche", wakipeleka pamoja nao, kutoka gereza, Padri Bosh na frera Damiano: wanatafuta radio ambayo Mapadri walikuwa wakiongoza "pilotes"; hawakupata kitu; Padri Bosh na frera Damiano walilazimishwa kukaa chini, bila vyatu na bila mifuko ya miguu (chaussettes); wafrera wakongomani walipashwa kurudia chumbani mwao. Kisangani "rive droite" ilikuwa chini ya utawalo wa Waaskari wa nchi. Utawalo wa Wamulele ulikuwa katika "rive gauche" tu. Padri Bosh alipigwa vikali kichwani na katika mabega. Kiisha watu wote wa Ulaya walirudishwa katika gereza; Wamulele walisindikiza Mapadri, Wafrera na Masera mpaka gereza na milio na matendo ya kuwaogopesha. Wafrera wacongomani walibakia katika Misioni.

Ilichaguliwa kama vile gereza nyumba ya msimamizi wa CFL (société de transports par train), karibu na Misioni. Katika nyumba hii ilikuwa duka ya matumizi ya askari (cantine).

“Cantine” ilikuwa katika giza na chepechepe; kulikuwa tu tundu 4 kwa kupumua. “Cantine” ilikuwa pia choo chao. Katika “cantine” walifungwa Mapadri, Masera na Wafrera; hakuna namna ya kukaa chini, wamoja wanabakia wima. Kwa zamu wanajilaza chini, kwa zamu wanaenda kupumua katika zile tundu nne; cantine ilikuwa pia choo cha wafungwa. Hata wafrera wacongomani walifungwa katika cantine. Wafungwa kwa jumla walikuwa 29: Mapadri 3: Trausch, Schuster na Bosh; wafrera 2 wa Ulaya: Henri Vanderbeek na Damiano Brabers; wafrera wacongomani 3: Richard Mobanza, Cyprien Dupou, na Jean Marie Likosi; Masera 7 ya Ubuntu; masera 4 “Dominicaines”; masera 2 “Franciscaines”; jamaa 2 ya “Pasteurs Protestants”: Harrison, na bibi na watoto 4; bwana Taylor, bwana Cool, mlimaji wa Ubuntu.

Kiisha Wasimba walimkamata pembeni Frera Richard kwa kumlazimisha abaki (violer) bikira mmoja; Frera alikataa, na alizarauliwa. Kiisha ilikuwa zamu ya frera Damiano, yeye pia alikataa. Kiisha zamu ya Padri Trausch na Frera Henri. Masera wote walikataa. Wasimba, katika hasira kubwa, wlitelemuka katika “cantine”, walitenga masera mmoja na wengine kwa ngumi, walimbeba juu, walimpatia kwa wasimba 4. Ndiyo vile kwa ajili ya masera wote (masera 13, pamoja na masera 3 ya Yanonge, kwa jumla masera 16 walibakwa na Wamulele). Wakati bikira mmoja anatelemuka, na machozi, na anaregea, ni zamu ya mwengine. Masera wote waliharibishwa, ila bibi ya “Pasteur” alipona, sababu alikuwa mzee. Wafungwa wanateswa na njaa na kiu. Frera Jean Marie alinunua kwa askari maji kidogo kwa 200 franka: wote walikunywa kidogo. Siku 26 Novemba wafungwa walibakia katika “cantine” wakiongea, kulia na kusali. Kopo ya maji ilipanda bei. Saa kumi ya mngaribi, kutoka Yanonge ilifika gari kwa kuleta wafungwa wengine: Mapadri 3: Vanden Vegt, Verberne na Newkamp; tena masera 3 wa Yanonge. Hesabu ya wafungwa inaongezeka: watu 35. Mapadri hawa na Masera walilazimishwa kuvua manguo mebele ya watu, na kubakia na suruali (caleçon) tu, na kutembea miguu kanya. Wakifika kwa gereza, Mapadri wanatelemuka katika “cantine”, masera wanangoja juu, chombo cha furaha na ujeuri ya Wamulele. Saa

kumi na moja wote tulipanda juu, katika chumba kuu, na Mkubwa wa Wamulele alisema:

> "Mlifika katika Congo si kwa kuhubiri Enjili, ila kwa kufanya politique chafu. Tutawapiga masasi nyinyi wote. Nanyi frera wacongomani muko waasi, marafiki wa Tchombe. Kwanza mtawazika wenzenu, kiisha tutawaua na kuwatupa katika tundu la wote, pamoja na wenzenu".

Hapo walianza kupiga masasi juu ya wote, isipokuwa wafrera wakongomani watatu, bibi ya "Pasteur" na watoto wake 4. Wakati wote walikuwa chini, walilazimisha wafrera wabebe maiti nje ya chumba, katika baraza. Wakati wafrera wanapitisha mwili wa mmoja mmoja, Wamulele walikuwa wakikata koo ya wale wasiokufa bado. Padri Schuster alionekana mfu mbele ya Wamule, hawakumkata koo, alipelekwa na wafrera katika fungu la maiti, lakini alikuwa mzima. Kiisha kutosha maiti nje, katika baraza, Wamulele walitaka wafrera 3 watupe maiti ya wenzao katika mto Congo, uliokuwa mbali kilometri moja. Usiku unakuja. Frera Richard anaomba kungoja kesho kwa kutupa maiti katika mto. Bikira mmoja, Margarita, hajakufa bado, akisikia yale maneno, anamwita frera na kumwambia: "Ee frera, tafazali unitupe mu maji usiku huo; napenda zaidi". Pale pale Wasimba wanakuja wanakata koo ya Margarita. Wakati wafrera wanaleta mwili wa bikira mmoja, Olimpya, nje, yeye alirudishwa ufahamu; alitosha katika kidole chake pete, tena aliondosha pete ya Mama Mkubwa aliyekuwa pamoja naye, alizipatia frera na kusema: "Tia hayo katika mfuko wako"; msimba anakuja kwa kukata koo ya bikira huyo pia. Olimpya, kiisha kufungua vizuri koo, alimwambia simba "Ngoja kidogo… sasa ndiyo kata".

Na simba alikata koo ya Olimpya. Wakati wafrera wanapeleka nje mwili wa P. Ten Bosch, waliona kama Padri hajakufa, Padri mwenyewe aliwaambia wafrera: "Ndugu zangu, sitapona tena, miguu yangu inaoza". Wote walikuwa wakilalamika, wakisali sala fupi. Wamoja wanawaambia: "Wandugu, mtutupe mu maji katika mto". Padri Schuster pia alipona; wafrera hawakuona hata kama Padri hakuwa tena pamoja nao.

Mwisho wafrera wacongomani walifungwa tena katika "cantine". Kesho yake, 27 Novemba, wafrera hawakuweza kutupa maiti katika mto Congo, sababu "Parachutistes Belges" walikuwa wakipiga masasi katika "rive gauche", kutoka "rive droite". Wafrera waliomba ruhusa ya kuchimba shimu kubwa kwa kuzika kikristu Mapadri na Masera; walitumika siku moja na jembe la kizungu ya zamani. Mangaribi walizika maiti mamoja (wafrera hawakumbuki maiti ya nani yalitupwa katika shimu); waliacha shimu wazi kwa kuendelea kuzika kesho yake. Siku 27 Novemba wafrera walikuwa na mchoko mingi; waliomba ruhusa ya kuenda kwa "Commune" kwa kuomba gari na watu kwa kuweza kuwasaidia. Walipata pia ruhusa ya kutafuta chakula kwa ajili yao, na kwa ajili ya bibi ya "Pasteur" na watoto 4. Wasimba 2 walisindikiza Frera Richard na Jean Marie, mpaka Misioni. Frera Cyprien, bibi ya "Pasteur" na watoto 4 walifungwa tena katika "cantine".





Wenye Heri Spoto na Anwarite

## Mwenye Heri Marie-Clémentine Anwarite Nengapeta

Anwarite alizaliwa tarehe 29 Novembre 1939, pa Wamba, katika jimbo la Haut-Congo. Baba yake, Amisi Badjulu, alikuwa askari, mama yake Isude Julienne. Alipobatizwa mwaka 1943 alipewa jina la Alphonsine. Tangu utoto wake alifahamisha nia ya kuwa bikira, lakini mama yake hakumwitikia. Anwarite alipenda sana kuwasaidia wazee, wagonjwa na watoto. Alipendelea sana kusali. Alizoea kuwapokea vizuri wageni.

Siku moja mabikira walipokuwa wakipita kijijini kwa kuwatafuta mabinti watakaoanza maisha ya kitawa, Anwarite akaingia, kwa uficho, ndani ya gari ya masera, na akapelekwa Bafwabaka, bila ruhusa ya wazazi. Basi, wazazi wa Anwarite hawakufika kumchukua kwa kumrudisha nyumbani. Hapo Mabikira walimwacha Anwarite aendeleshe maadibisho na tarehe 5 Augusti 1958, Anwarite pamoja na wabinti wengine, akatoa naziri zake za kwanza za utawa. Muda wa maisha yake Anwarite alionekana mwenye juhudi kazini na mwenye kupenda watu wote. Anwarite alikuwa na mapendo makubwa kwa ajili ya Bikira Maria. Alipouawa alikuwa akificha mfukoni mwake sanamu ndogo ya Bikira Maria.

Mwaka 1964 fujo ya vita ikazuka (apparait) nchini Congo. Tarehe 15 augusti waasi-Simba wakafika Wamba, na tarehe 29 Novemba 1964 waasi-Simba wakafika mpaka Bafwakaba, wakaingia katika nyumba ya mabikira na wakawalazimisha wapande katika gari lao, ili wawapeleke Wamba. Njiani, pa Yube wakuu wa waasi wakaamuru misalaba iondoshwe vifuani mwa mabikira. Kutoka Yube, pahali pa kupelekwa Wamba, mabikira wakapelekwa Isiro na kufungwa ndani ya nyumba moja “maison bleue”. “Colonnel” Ngalo akatuma askari wamletee Anwarite ili awe mke wake. Anwarite akakataa kwa nguvu zake zote, akisema: “Siwezi kuitika hata siku moja maishani mwangu”. Mwasi mmoja akatafuta kumwogopesha, akamwambia: “Ikiwa

haupendi kuwa bibi wa Colonnel wetu, tutaua mama Leontine, mmoja kati yenu". Anwarite akajibu: "Sababu gani kumwua dada Leontine? Kama ni vile, basi, mniue mimi peke". Hapo colonnel Ngalo akamweleza mwenzake colonnel Olombe, akisema: "Yule bikira Anwarite ananipendeza na ninahitaji awe mke wangu; basi, ikiwezekana, umlazimishe aitike, aje kwangu". Olombe akasema: "Usiwe na shaka, mwenzangu, nitamletea kwako kwa pigo" Anwarite akasema: "Ikiwa nitakufa kwa sababu ya ubikiwa wangu, basi, nife. mimi niko bikira na nimefanya agano na Mungu". Olombe alikamata Anwarite pamoja na bikira mwengine, akawaingiza katika gari lake; nia yake ilikuwa kumpeleka Anwarite kwa colonnel Ngalo, na yeye, Olombe atamtwaa bikira mwengine awe bibi yake. Olombe, alipoingia nyumbani kuchukua funguo ya gari, mabikira 2 walitoka kwa gari kwa kukimbia. Olombe alijaribu kuwaingiza tena ndani ya gari; mabikira walikataa. Hapo Olombe alianza kuwapiga na nguvu zake zote. Alipopigwa na tako la bunduki kichwani, Anwarite akasema: "Ndivyo nilivyotaka". Kiisha akanyosha uso na kumwambia Olombe: "Nakusamehe, kwa sababu haujui utendalo". Olombe akaendelea kuwapiga mpaka wote wawili wakazimia. Olombe akauliza watu wake: "Muna bunduki? Muna silaha gani?" Wakamjibu: "Tuna visu viwili virefu".

Hapo Olombe akaamuru mmoja kati ya Simba: "Unaona yule Anwarite, umchome kwa kisu chako, ukakipenye mpaka moyoni". Pale pale yule Simba akamrukia Anwarite na akachoma ubavu wake, kwa kisu, mara tano. Usiku wa tarehe 1 Desemba 1964 bikira Anwarite akatoa roho. Siku moja mbele ya kuuawa, tarehe 30 Novemba, aliandika hivi katika buku lake: "ushahidi wetu juu ya usafi wa moyo, na Bwana Patris".

## Mwenye Heri Francesco Spoto

Francesco Spoto alizaliwa siku 8 Yulai 1924 pa Raffadali (Agrigento, Italia). Anaingia katika Seminario ya "Serviteurs des pauvres" pa Palermo. "Les serviteurs des pauvres" wanaitwa pia "Bocconisti", maana yake "tonge ya mkate kwa ajili ya maskini". Siku 22 Yulai 1951 alipata Upadirisho, kwa mikono ya Cardinal

Ernesto Ruffini. Katika “Chapitre Général” ya “Serviteurs des Pauvres” ya mwaka 1959 alichaguliwa kuwa “Supérieur Général”: alikuwa na miaka 35. Alishangaa sana juu ya uchaguji huo na aliandika hivi kwa mama yake:

> “Nilitafuta kuishi katika uficho na unyenyekevu. Lakini nakubali mapenzi ya Mungu. Natia kitumaini changu katika Bwana atakayeniwezesha niwe na afya nzuri, utaratibu na hekima katika matendo yangu. Yeye aliye na nguvu zote atanisaidia katika uzaifu wangu”.

Siku 4 Augusti 1964 alifanya safari kwa kutembelea wandugu wake watatu waliounda Misioni ya Birindi (Ituri, Congo).

Siku 3 Desemba 1964 Wamisionari « Serviteurs des pauvres » 3 walikamatwa na Wasimba pamoja na Padri Spoto, Mkubwa wao. Padri Spoto alikimbia, miguu kanya, akijisumbua kwenda huko na huko, katika pori. Alisimama na mchoko na uzaifu; akapiga magoti, alisali: «Ee Bwana, nakutolea maisha yangu, lakini uokoe wandugu wenzangu ».

Siku 27 Desemba 1964, alipokuwa na miaka 40, sababu ya mapigo ya damu na vidonda aliyopata kwa Simba, alikufa. Lakini wandugu wake watatu, kiisha siku chache walionekana katika uhuru.

Siku 21 Aprili 2007, na ruhusa ya Papa Benedikto XVI, alitajwa mwenye heri.

# SEHEMU YA PILI: FRERA VITTORIO FACCIN



"Ni mashahidi wenu;
mwandike historia yao;
mheshimu maiti yao".

Ndiyo maneno ya Mtakatifu Paulo wa VI, kwa Askofu wa Uvira Danilo Catarzi, wakati alimwambia papa kama wandugu wanne waliuawa kwa ajili ya Kristu, katika Congo. Tukisoma historia ya mashahidi wa Enjili katika Congo, mwaka 1964, tunakumbuka "Historia ya Mashahidi ya Yesu Kristu", mwanzo wa Eklezya.

Kifo cha Frera Vittorio Faccin, wa kwanza kwa kutoa uzima, hakikuwa msiba wa rafla, ila kilele ya maisha yote ya mtu anayejitolea kila siku kwa Yesu Kristu.

Kijana wa matumaini mazuri, tabia heri, anakomaa vizuri, anajionyesha vizuri, mwenye kicheko kila mara, wazi, bila wongo, mkarimu, ahadi nzuri kwa wakati ujao: kwa jamaa ya Waxaveriano na Eklezya, na kwa watu wote walioaminiwa kwake. Fazila hizo zinakamilishwa wakati, katika furaha na juhudi ya ujana, anajitolea kama vile sadaka katika Congo.

Vittorio alizaliwa siku 4 Yanuari 1934 katika mji Villaverla (Vicenza). Wazazi wake: Giuseppe Faccin, mlimaji, na Giuditta Zanin, mama wa nyumba. Vittorio alikuwa mtoto wa tatu kati ya wandugu 6: Silvia, Bortolo, Vittorio mwenyewe, Dante (alikufa alipokuwa na miaka tano), Antonio, Dante. Siku mbili nyuma ya kuzaliwa, siku 7 Yanuari 1934, Vittorio alibatizwa; alipata Usabitisho siku 21 Februari 1943. Kweli Mungu, katika jamaa ya Vittotio, ni kwake "chez Lui". Vittorio anazoea kusali Rosaryo; dada yake Silvia Maria, wakati anatengeneza kitanda cha Vittorio, kila mara anakuta Rosaryo chini ya takia.

Kiisha masomo ya misinji, Vittorio anasaidia wazazi. Jamaa inahama kutoka Villaverla kwa kuenda kukaa Nonantola, karibu na Modena. Alipokuwa na miaka 16 Vittorio anaonyesha nia yake ya kuwa Misionari; lakini alingoja kwa kusaidia jamaa katika kazi ya mashamba. Mwisho wazazi walimpatia ruhusa ya kuingia katika jamaa ya Misionari Xaveriano.

Mahaba (tendresse) ya Vittorio kwa ajili ya jamaa yake. Vittorio alikuwa akipenda sana jamaa yake; tangu Congo anawaandikia maneno ya utulivu na ya mapendo:

> "Niliposoma barua yenu, nilisikia mshtuko ndani ya moyo; muna kazi mingi na hamuwezi kupata watu wa kazi kwa kuwasaidia katika mashamba. Nakumbuka sasa miaka tulipokuwa wote pamoja karibu na meza. Leo, kiisha miaka 12, mnabakia watatu tu karibu na meza. Wazazi wangu wapenzi, nani angewaza juu ya tukio hilo? Ninyi mliotupatia uzima, mlibakia tu na ukumbusho wa utoto wetu. Neema ya Mungu inawapatia nguvu kwa kushinda magumu ya namna hii. Kila siku tunabakia pamoja katika sala; kila saa nawaza juu yenu. Na wewe ndugu yangu Bortolo, nakuambia aksanti, aksanti mara elfu, sababu ya majitoleo yako na mapendo yako kwa ajili yetu sisi wote. Ningependa sana kuwa karibu nawe kwa kukusaidia, lakini siwezi. Nakuombea ili Mungu awe karibu nawe na neema yake".

Vittorio anajifanya karibu, wakati ndugu mmoja anagonjwa: "Ugonjwa wa Dante unaleta huzuni kwa wote, hasa kwenu, wazazi wetu. Katika Enjili tunapata jibu. Kama Baba yetu anashurulika na ndege ya angani na maua ya shambani, zaidi na zaidi atashurulika na sisi watoto wake. Sisi kama watoto wa Mungu na warisi wa Paradiso, tunapashwa kuwa na shuruli moja: kuishi kila mara bila zambi kubwa."

Vittorio anaanza utume wa Misionari katika jamaa yake. Misionari wa kweli anashurulika na wokovu wa watu wote. Mbele ya kushurulika na watu wa mbali, anashurulika na watu wa karibu, jamaa yake. Kutoka Afrika anamwandikia ndugu yake Dante, bila woga, bila haya, wazi wazi:

> "Ukumbuke kama una roho moja ya kuokoa; kila mtu anapashwa kuokoa roho yake; kama roho yetu inapotea, ukomo wa maisha unapotea. Sitakuambia: acha kazi sababu ya vishawishi; uombe msaada wa Mama wa mbingu, upate kuepuka zambi. Kama mwili wako ni safi, hata roho yako ni safi. Watu wawili wanaweza kukusaidia: Padri Mwongozi wa roho na mashauri ya mama yetu, anayejua vizuri maisha ya watu. Usiache kazi, ubakie kwa kutoa mfano mzuri. Usishindwe, ila uwe mshindaji. Mwili wetu ni Hekalu la Roho Mtakatifu. Uwe mhodari, uutumainie msaada unaotoka juu. Katika sala zetu tuombeane".

Anamshauria pia ndugu yake Antonio, kutoka Afrika:

> "Kwako, mpenzi wangu, nakutakia mema mazuri sana, katika sala kwa Yesu na Maria. Ubakie kila mara mkristu mwema, uwe mhodari katika imani ya wazazi wetu. Kama unaungama Yesu mbele ya watu, Yesu atakuungama mbele ya Baba yetu wa mbinguni. Siku ngapi zinabakia kwa kutimiza utumishi wako wa askari? Uwe na moyo, mpenzi wangu, kwa jina la Bwana Yesu".

Vittorio alikuwa na miaka kumi na saba; aliisha acha masomo tangu miaka nne kwa kutumika katika mashamba. Sasa anaomba kuingia katika jamaa ya Misionari Xaveriano. Ushuhuda wa Padri Mkubwa ya Parokya yake ni mzuri na wazi:

> "Vittorio Faccin ni mtu wa imani na mwendo wake ni mzuri. Wakati huo wa mwisho alionyesha nia ya kujitolea kwa Mungu kama vile Misionari".

Vittorio aliingia katika jamaa ya Misionari Xaveriano, pa Cremona siku 19 Oktoba 1950. Mapadri wa Cremona wamamshuhudia Vittorio na maneno haya:

> "Vittorio Faccin: tabia ya mwenye woga kidogo; mtu wa sala na imani. Anadumu kwa uvumilivu katika kazi; mnyenyekevu, mwenye adabu, mtii; akili ya kawaida, mapenzi mema kwa kujifunza".

Kiisha mwaka moja pa Cremona, Vittorio anakubaliwa kuanza Noviziati pa Piacenza na Parma, kwa kuwa Frera Misionari. Siku 8 Desemba 1952 anajitolea kwa Mungu kama vile Frera Misionari, kwa njia ya naziri ya umaskini, usafi wa moyo, utii na ya misioni.

Tangu mwaka 1953 mpaka 1955 Frera Vittorio ni Mlinda mlango (Portier) katika nyumba- mama ya Parma: mlango wazi wa nyumba-mama ya Parma ulikuwa mfano wa moyo wazi wa Vittorio kwa kuwapokea watu, kwa mapendo, furaha na unyenyekevu. Waxaveriano wanamkumbuka Vittorio katika kazi yake ya "Mlinda mlango" na maneno hayo:

> "Namkumbuka kama vile Mlinda mlango katika nyumba-mama ya Parma. Anajionyesha vizuri, mwenye kicheko na adabu, kila mara mfurahivu, mustarehe raha, anafika kwa saa; alikuwa anawatumikia wote na juhudi na adabu nzuri. Kulinda mlango kwa Vittorio, mshujaa ya miaka 22, mfurahivu na mwenye nia ya kutangaza Enjili duniani kote, haikuwa kazi nyepesi; lakini aliikubali na unyenyekevu na utii. Vittorio anatumika hata usiku.
>
> Kila siku matendo yale yale: kufungua, kufunga mlango, kuwapokea watu, kuwasindikiza, kujibu kwa "téléphone", kila mara

tayari, karibu na mlango; kuwa macho na kuwa na utaratibu. Mshahara wa kazi alipata kwa Mungu peke yake; watu hawazoei kuwa na shukrani kwa mlinda mlango."

Tangu 1956 mpaka 1957 Vittorio alikuwa vile vile na ile kazi ya Mlinda mlango katika nyumba ya Xaveriano wa Desio (Milano). Alipokuwa pa Desio Vittorio alishtakiwa wongo kama aliiba. Sababu hakuwa na kosa, angeweza kujitetea, lakini alinyamaa kwa kuepuka haya ya watu wengine wenye kosa, na kwa kulinda umoja wa jamaa. Mwenye haki alikubali malipizi; alijitwika kosa na malipizi ya ndugu mwengine: kurudia tena Parma kwa kazi ilei le ya Mlinda mlango, tangu 1958 mpaka 1959.

Hata wakati alikuwa na kazi ya Mlinda mlango Parma na Desio, huba yake kubwa ilikuwa: kutumwa katika Misioni. Siku kuu ya Noeli 1954 anamwandikia P. Giovanni Gazza, Mkubwa wa Xaveriano wote:

"Leo, siku kuu ya Noeli, mimi Vittorio Faccin, naomba unitume katika Misioni unayopenda. Mimi mtoto wako wa mwisho".

Kiisha miaka nne, siku 21.7.1958, anaomba tena kwa Padri Mkubwa mpya Giovanni Castelli kutumwa katika Misioni: "Nakuomba usikilize ombi langu la kutumwa katika Misioni".



Nyumba ya mapadri pa Baraka

Ombi la Vittorio linasikilizwa na siku 3 Desemba 1959 anatumwa kama Frera Misionari katika Congo. Maneno ya Mtakatifu Guido Maria Conforti yamsindikiza Frera, kama vile mashauri na kama unabii juu ya kifo cha Vittorio:

> "Mtahakikisha Neno la Mungu na ushuhuda wa maisha yenu matakatifu, kwa matendo ya huruma, kwa roho ya kijitolea, kwa ushujaa wa kufa kama ni wito wenu. Damu ya mashahidi kila mara ni mbegu wa kutoa matunda. Magumu mtakayopata katika kazi yenu ya kitume yatakuwa nyepesi, mkitazama ukomo: kufa kwa ajili ya Yesu".

Siku kuu ya Mtakatifu Fransisco Xaveri, 3 Desemba 1959, alipokuwa na miaka 25, Vittorio anafunga safari kwa kuenda Congo. Mwenzake wa safari, na kiisha mwenzake wa kifo kwa ajili ya Yesu, P. Giovanni Didonè. Misioni ya Vittorio ni Baraka. Siku tatu kiisha kufika Baraka, anawaandikia wazazi kwa kuwaonyesha furaha ya kuwa Misionari.

> "Siku 6 ya Desemba, 1959, saa kumi na moja na dakika makumi nne ya usiku (5h40), naanza safari pamoja na Padri Vagni. Kanisa ya mji tunapoenda ni ya mianzi. Padri anasoma Misa: watu 200 wanakomunika, na watu 100 walikosa komunyo, sababu hostia ziliisha. Pa saa tano nanawa katika ziwa Tanganika. Siku 7, kama vile mdereva, nasindiza mapadri katika nafasi yao; safari ya 760 Km. Siku 8 Desemba, katika rala ya kanisa (sacristie) ya "Pères Blancs" wa Bukavu, mbele ya wandugu wawili, natoa tena naziri. Siku ya kwanza, 14 Desemba, narudia Baraka. Siku ya pili naanza kufahamiana na vijana wa masomo; wananipokea vizuri; tunacheka mingi pamoja; mimi nachanga swahili na kifransa. Pole pole naanza kuongoza kundi la watu kwa kufanya kazi moja moja. Kuwa katika moyo wa Afrika kwangu mimi ni kama vile ndoto; ni nafasi nzuri sana kwenye niko. Katika ziwa ya Tanganika kuna kisiwa-nusu (presquile), Ubwari: kwa kuwatembelea wakristu tunaenda hako na mtumbwi. Wazazi wapenzi hamuwezi kuwaza furaha tunayo hapa,

nikiona kama naweza kujitolea kwa ajili ya wandugu hawa wasiomjua bado Kristu".

Pa Uvira Frera Vittorio alijitoa kwa Mungu na kwa wandugu kwa maisha yake yote, ndiyo Naziri ya milele aliyofanya siku 8 Desemba 1962. Vittorio alijitayarisha vizuri kwa hii siku kuu; barua yake inaonyesha namna gani alitamani kujitolea kwa Bwana maisha yake yote:

"Kama Mungu anapenda, siku 8 Desemba nitafanya Naziri ya milele. Wakati mnanikumbuka mbele ya Mungu, mumwambie anifanye wake kabisa, bila vizuio. Mnikumbuke mbele ya Bikira Maria. Najitayarisha kwa mafungo ya roho. Yesu mwenyewe aliyeniita niwe mfuasi wake, atanipatia neema ya kumfuata mpaka mwisho. Natamani hii siku ije haraka kwa kujitolea kwa Yesu kama vile sadaka kwa wokovu wa watu".

Ile siku 8 Desemba, anamshukuru Mungu:

"Sifa kwa Mungu mwenyezi, sifa kwa Mwana wake Yesu Kristu aliyekufa msalabani kwa ajili yangu, sifa kwa Roho Mtakatifu aliyenichagua nimfuate Yesu kwa karibu. Vijana wengi wa Uvira walihuzuria ibada ya naziri, kwa kumtukuza Mungu".

Karibu maisha yake yote ya misionari, Frera Vittorio alitumika pa Baraka: 1960-61; 1963-1964 kama: msimamizi wa watu wa kazi, makamo ya "économe", mwongozi wa vijana, "économe". Mwaka 1962 Frera Faccin alitumika katika Misioni ya Kiringye.

Mwaka 1962, mwezi wa sita, tunamkuta Frera Vittorio katika Seminario kubwa ya Murhesa kama Mwalimu pamoja na waalimu wengine wa nchi mbalimabli; Vittorio anaishi maisha ya kindugu pamoja nao na pamoja na Waseminarista wacongomani waliokuwa 46 ule mwaka.

"Tunapumzika pamoja; hatuulizani: unatoka wapi; mapendo ya Yesu yatusaidia kusahau kama tupo Wabeleji, Wafransa ou Waitaliana ao Wakongomani. Hapa tunasema kifransa kila mara."

Pa Baraka Frera Vittorio anaishi na anatumika pamoja na Padri Giovanni Didonè. Padri anasema kama Vittorio ni mkono wake

wa kuume, kitulizo chake, na yeye Didonè ni kitulizo kwa Vittorio.

Ukatekumeni ndiyo utumishi wa kwanza wa Wamisionari. Vittorio anaangalia Ukatekumeni na furaha kubwa na kitumaini: furaha kubwa ni mavuno, maana yake Ubatizo wa Wakatekumeni.

> "Hapa kwetu tuliisha anza tangu siku kumi, matayarisho ya Ubatizo. Watakaobatizwa siku ya tano ya Juni ni 80 Wakatekumeni, karibu wote ni watu wazima, tangu miaka 20 na kuendelea. Nawaalika ninyi wote msali kwa jili yao ili wawe wakristu wazuri, hasa wakati huo wa kungoja uhuru."

Safari katika misioni ni mingi sana kwa kukutana na wakristu na watu wote wa mapenzi mema.

> "Siku 7 Yuni 1960. Safari ya Vittorio pamoja na Giovanni Didonè, Padri Mkubwa ya Misioni. Kulamka: 4h45; kusali, Misa. Saa 8h30 tunaanza safari, saa 5 na gari; tunapanda mpaka milima ya 2500 metri. Hapa inafaa kujifunika vizuri, sababu ya baridi. Barabara inaisha. Ni saa kenda. Vijana wanatusaidia kubeba mizigo; saa moja ya safari na miguu. Njiani vijana wanasemezana kati yao "Frera ni mrefu sawa na sisi". Wakristu wanatupokea na zawadi: kuku na mayayi 4. Kibanda chetu kina vyumba viwili; wanatuletea maziwa ya ngombe; usiku, nilipokuwa kitandani nilisikia mtetemeko wa dunia, lakini kibanda chetu kilibakia wima. Kesho yake, 6.6.1960, Misa pa 8h30, si watu wengi wanafika. Karibu na kibanda chetu kuna kibanda cha Mkatekista; vile vile vyumba viwili, moja kwake, na ngine kwa mbuzi zake; vibanda hapa vinajengwa na mafi ya ngombe na mianzi. Siku 9 Yuni 1960 tunaendelea katika safari yetu, tunafika katika mji mwengine. Padri anaanza kuungamisha wakristu, mimi naangalia buku ya daftari ya wakristu na Wakatekumeni. Pa saa 10h30 Misa; kiisha Misa padri anabatiza watoto na anampokea mgonjwa mmoja; mimi nafanya mapepeto (examen) ya wakatekumeni; tunaanza safari ya kurudia, tunafika Mikelati; usiku nalala na manguo yote sababu ya baridi na ya upepo kali.Tunatelemuka, upepo na baridi zinapunguka. Njiani tunakuta mito mbalimbali, tunasimama, tunanawa na tunaendelea. Siku 22 Yuni tunafika Baraka, kiisha siku mbili ya kazi ili gari yetu iweze

kuendelea mpaka Misioni. Nafurahi sana sababu ya hii safari. Tulipata magumu; namshukuru Mungu sababu ya kuyashinda. Ya lazima ni mapendo ya Mungu anayetuzidisha furaha ya moyo".

Kazi kubwa aliyofanya Vittorio kwa ajili ya misioni ya Baraka ilikuwa Kanisa npya:

"Sasa mnauliza nilifika Baraka kwa kufanya kazi gani. Misioni yetu inakosa Kanisa. Askofu alinituma hapa kwa kujenga kanisa. Kwa sasa husoma Misa chini ya mti; Mungu kweli ni mwema; mwaka huo haikunyesha hata mara moja wakati wa Misa, lakini mwaka uliopita, karibu siku ya Mungu zote ilinyesha. Vipimo vya kanisa npya: urefu 32 metri, upana 14 metri, uketo 5 au 6 metri. Siku 24 Mai (1963) tulibarikia jiwe la kwanza. Sasa tunakosa sarufi (ciment) sababu vivuko vya Tanganika vinafunikwa na maji; tunapashwa kusimamisha kazi."



Kalambo 08.12.1962: Naziri ya milele ya fr. Faccin

Unyongonyongo unaanza kuambukiza watu; wakubwa wa nchi wanakataza mikutano ya vijana: scouts na Xaveri.

> "Siku ya nne, 2 Februari 1961, ilishuka mbele ya nyumba yetu "élicoptère de l'O.N.U"; alishuka askari mmoja, anamwendea P. Adriano, anatuuliza kama tunapenda kukimbia na kuacha Congo pamoja na yeye. Sisi wote tunakataa; vijana na watoto wengi wanafika kuangalia "élicoptère"; "élicoptère" iliruka na sisi tuliweza kula, bila masito. Kiisha, upande wa 15h30 gari ya waaskari inafika kwa Misioni; wanatuuliza juu ya "élicoptère" na barua tuliyopokea.
>
> Habari ya barua ilikuwa ya wongo; wanatazamia vitu vyote vya Misioni, wanaiba litri 160 ya "essence", wanatubeba katika njia zote za Baraka, kiisha wanaturudisha kwa Misioni; naanza kunawa, gari ya pili inakuja na kundi la waaskari (20), wananitosha nje; wanatupeleka gerezani: mimi, P. Knittel, P. Adriano na P. Costalonga".

Vittorio anafurahi:

> "Katika moyo wangu nilikuwa na furaha kubwa, sababu nilijisikia (kama vile wa mwisho) katika kundi la wale wanaoungama imani".

Mapadri wengine wanarudishwa kwa Misioni, lakini Vittorio anarudishwa gerezani. Ile siku mvula ulinyesha mingi pa Baraka. Mapadri wote na Vittorio wanafungwa na wanapelekwa Uvira na kiisha Bukavu, wajitetee mbele ya Mkubwa Kasamura. Wanabakia gerezani mpaka siku ya kwanza, 6 Februari 1960. Kasamura, katika Shauri ya Jimbo, anakata maneno ya wafungwa wetu.

Waliwapatia barua ya ruhusa ya kurudia Baraka, isipokuwa P. Adriano anayetajwa "persona non grata". P. Knittel anapumzika kidogo pa Bukavu, kiisha anarudia Ulaya. P. Costalonga na Vittorio wanabakia Uvira, hivi Missioni ya Baraka inafungwa kwa muda. Pa Uvira furaha ya kuweza kukomunika tena, kula katika meza inyofunikwa na kitambaa safi.

Siku 13 Februari 1961 Vittorio pamoja na Padri Vagni na Padri Didonè wanarudia Baraka; Padri Costalonga anabakia Uvira. Wakristu walilinda vizuri Misioni ya Baraka na walipokea Mapadri na furaha. Wakristu wanashiriki huzuni ya Mapadri, wakisema "Mlifanya ubaya gani, hata wawapeleke mbali?"

Kiisha kifo cha Lumumba magumu yaongezeka. Siku moja ya 1961, saa 4 ya usiku(10h) gari ya waaskari inafika Baraka kwa kuhesabia na kuwakinga Wazungu; mapadri wanaingia katika gari na wanapelekwa mpaka Fizi, na pa Fizi kwa kulala walipelekwa kwa gereza. Wakubwa wa Fizi waliwaruhusu Mapadri kurudia katika missioni yao na kukingwa na waaskari wa nafasi. Kweli Vittorio alionja huzuni ya gereza zote, tangu Fizi mpaka Bukavu.

Sababu ya magumu Misioni ya Baraka inafungwa muda wa miezi mitatu: mapadri watatembelea wakristu mara moja moja, kutoka Uvira. Vittorio anaacha Baraka na anatumwa Kiringye. "Elicoptère" iliyoshuka Baraka iliwaletea mapadri magumu hayo yote.




Baraka 02.02.1961; Elicoptère de l'ONU

## SEHEMU YA TATU: PADRI LUIGI CARRARA



Ilikuwa siku 28 Novemba 1964, asubui, P. Luigi Carrara anapiga magoti, anasali, anabarikia maiti ya mwenzake Frera Vittorio, tendo kubwa ya mapendo na ya huruma; kiisha anapigwa masasi kifuani na anakufa.

Juma moja mbele, papa Mtakatifu Paulo wa sita alitangaza barua “Lumen Gentium”, tunaposoma kama “Wakristu wote wanaitwa kuwa watakatifu”. Papa alisema juu ya tendo la kuuawa kwa ajili ya Kristu kama vilen “ushuhuda kubwa sana wa mapendo mbele ya watu wote hasa mbele ya watesaji”.

Ndiyo historia ya kijana mmoja, misionari, aliyejitolea kwa Afrika, kwa kuwa mtumishi wa Enjili ya huruma. Padri Luigi ni mmoja katika ile kundi ya mashahidi walionyunyiza bara la Afrika na damu yao, ili itoe matunda.

Kweli muuaji wa P. Luigi, hakuiba maisha yake; Luigi aliisha toa mbele. P. Amato Dagnino, Mwalimu wa P. Luigi, aliwaandikia wazazi wa Luigi, mbele ya Naziri ya milele maneno haya: “Luigi wenu ni mwema kama vile mkate; nawaza kama atakuwa mtakatifu kabisa. Sifa gani! Furaha gani ! Baraka gani kwa ajili yenu !”

+ Francesco Beschi, Askofu wa Bergamo

Luigi Giuseppe Carrara alizaliwa katika mji wa Cornale di Pradalunga (Italia, Bergamo) siku 3 marsi 1933. Wazazi wake: Giuseppe Carrara na Rossi Felicita; walizaa watoto wanne, wote wanaume. Siku tatu nyuma ya kuzaliwa Luigi anabatizwa. Mama yake Felicita anasema juu ya mtoto Luigi (Gigi).

"Nilishurulika sana na Gigi, alipokuwa na miaka kenda ao kumi. Mara moja moja, usiku, kiisha kulala vizuri, anaamka kwa rafla, kama angeshikwa na woga na kitisho. Hapo, pole pole, bila kuamsha wadogo wake, anafika kwa kujikinga, mwisho wa kitanda changu. Halafu naamka kwa rafla, na namkamata katika kitanda chetu. Analala haraka na amani na hivi msukosuko unaisha. Tendo hilo ilidumu kidogo; sikuweza kujua sababu. Katika masomo aliendelea vizuri. Alikuwa anahitaji hewa na mwangaza, afya yake ilikuwa nzuri.

Alipokuwa na miaka kumi na nne, sisi wazazi, kadiri ya desturi zetu, tulitafuta mtu ili amfundishe Gigi kazi moja, lakini karibu na nyumba, sababu yeye alikuwa mtoto na bila kujua maisha ya watu. Nyumbani, asubui na mangaribi, kila mara tunasali, kiisha tunaongeza sehemu ya Katekismu. Mimi na bwana wangu tulianza vile tangu siku ya ndoa yetu. Mara moja moja watoto wetu wanasinzia wakati wa sala; nawaza: watoto wangu wanalala, na sala midomoni".

Mama wa Luigi anahadisia juu wito wa kuwa Misionari wa mtoto wake:

"Siku moja alifika nyumbani mwetu Padri Mkubwa wa zamani Ercole Ferri na alituambia: "Mtoto wenu Gino anapenda kuwa Padri Misionari". Tulishangaa sana.Kwa kunituliza nilimwendea Padri Mkubwa wa sasa David Brugnetti. Pamoja na yeye na bwana wangu tuliwaza ya kama inafaa kumshauria Gino aingie katika Seminario, kwa kuwa Padri katika Diosezi. Luigi alikataa shauri hiyo na alikamilisha nia ya kuwa Padri Misionari. Na huzuni moyoni nilitayarisha mfuko, nilitia ndani mavazi kidogo, mabuku na bics, nilimsindikiza Gigi mpaka Pedrengo, nyumba ya Misionari Xaveriano kwa kuwaadibisha vijana wenye kutaka kuwa Misionari; vijana wanaitwa "apostolini", maana yake "mitume wadogo".

Padri Mkubwa wa Parokya anatoa ushuhuda mzuri juu ya Gigi.

Gigi anarudia nyumbani mara moja moja kwa kupumzika, kadiri ya desturi. Yeye mwenyewe anasema anafanya nini kila siku:

> "Kila siku: asubui napitisha saa moja na nusu ao saa mbili kanisani, sababu niko na wakati; mangaribi saa moja kwa kumtembelea Ukaristia Takatifu, kusoma, Rosaryo: kanisani; nyumbani sala zingine. Wakati ngine nasaidia wazazi".

Luigi tangu mwanzo alipenda kuwa Misionari na nia yake ilikuwa safi, bila kuichanga na nia zingine. Yeye mwenyewe anachungua wito wake na anaona kama ni moja tu na safi: kuwa Misionari.

> "Nilichungua vizuri wito wangu, tangu nilikuwa katika somo la tatu la juu. Niliingia katika nyumba ya Waxaveriano kwa kugeuka kuwa Misionari. Mwanzo sikujua vizuri kuwa Misionari ni nini. Lakini kiisha niliona Misionari wa mji wangu kuondoka kwa kuenda China. Halafu nilisikia huba kubwa sana ya kuenda mimi pia katika Misioni, ndiyo sababu niliacha mji wangu".

Luigi, bila haya wala kiburi, na unyofu, anasema wazi juu ya maisha yake ya sala na ibada:

> "Sala zangu nazifanya vizuri kila mara, hata wakati wa mafungo. Namwomba Bikira Maria, hasa katika sikukuu zake; nafanya mambo madogo madogo kwa kumwonyesha mapendo yangu. Kuhusu "méditation", nasikia mahubiri, nafikiri polepole, nasema nia ya kutimiza wakati wa mchana. Lakini usiku, mara moja moja nasahahu yote".

Luigi anajua tabia yake na fazila zake. Anasema wazi wazi:

> "Tabia yangu ni ya mwenye kiburi, nawaza vibaya juu ya wengine. Mwaka huo nilijikaza na niliweza kupata matunda madogo. Niko hakika kama usafi wa moyo ni zawadi ya Mungu kwa watu wachache, ni msaada kubwa kwa kujifunza na kwa kazi ya kitume. Kila mara natafuta kuepuka kushindwa na vishawishi, hasa vishawishi vinavyoharibu usafi wa moyo: naomba mashahuri kwa Wakubwa wetu. Nataka kumpenda Mungu na kujitolea kwake kabisa. Masomo yaendelea vizuri kwangu. Kama mwanafunzi singari, lakini napenda kuendelea vizuri zaidi, na msaada wa Mungu na wa Bikira Maria. Natamani kuingia katika noviziati. Najikatalia kusemasema na ulafi, najitolea kuhurumia, japo siwezi pale pale".

Mwaka 1953-1954 ni mwaka wa noviziati kwa ajili ya Luigi; aliishi mwaka mmoja katika mji wa "San Pietro in Vincoli".

Siku 12 Septemba 1954 Luigi anaingia katika jamaa ya Misionari Xaveriano, kwa njia ya naziri ya umaskini, utii, usafi wa moyo na kutangaza Enjili duniani kote. P. Mario Ghezzi, Mwalimu wa Noviziati anamshuhudia Luigi na maneno hayo:

> "Luigi ni kijana mzuri sana, excellent: anajitolea, anatii, ni mfurahivu; wenzake wanampenda na wanamwheshimu. Nakubali kwa utashi wangu wote atoe naziri".

Bikira mmoja, Margherita, wa mji wa Luigi, anamkumbuka Luigi na maneno hayo:

> "Namkumbuka Luigi, mbele ya Upadirisho, wakati wa mafungo; yeye alizaliwa mwaka 1933, na mimi mwaka 1935. Luigi alirudia nyumbani mara moja kwa mwaka. Namna yake ya kusali ilinistusha. Nilikuwa na nia ya kuongea naye; namgoja kanisani dakika kumi na tano, nusu saa, lakini yeye hatoki kanisani. Nilimtazama na uangalifu, nilikaza macho kwake: namwona kanisani katika hali ya sala na kumtazama Mungu; kiisha Misa namungoja, lakini bure, nachoka kumgoja anapotoka kanisani. Ninapomwona kusali kanisani katika marfaa ya tatu, ngambo ya kushoto, na mimi naambukizwa huba ya kusali vizuri, kama yeye. Katika namna yake ya pekee ya kuwa, kusema, na kutazama alionekana kama vile malaika. Namna ya kusali ya Luigi ilinishtusha".

Luigi alijitayarisha vizuri kwa kupata Upadirisho. P. Eugenio Morazzoni anakumbuka wakati huo.

> "Pole pole Luigi alizoea na vitabu, akitosha jasho. Sababu ya umri wake nilimtaja Mwalimu wa ibada (Cérémoniaire) ya kanisa yetu. Utumishi huo ulimpatia namna ya kuwa karibu zaidi na Yesu Ukaristia. Ibada yake kwa Ukaristia na Bikira Maria ilingara kwake kama mwanga wa pekee. Alizoea sana kusali. Mara mingi anaingia kanisani kwa kusali, kusafisha, kutia maua vizuri. Kanisa ilikuwa nafasii ya kupendeza. Upadirisho unapokaribia, Luigi alikuwa

akionyesha huba yake kubwa kwa kuondoka na kwenda katika Misioni".

Padri Martino Cavalca vile vile anatoa ushuhuda wake juu ya Luigi Carrara, ibada yake na fazila zake.

"Mara mingi, nikipita kanisani, namwona Luigi anapiga magoti mbele ya altare ya Ukaristia, akionyesha imani kubwa: siwezi kusahau. Fazila yake: unyenyekevu na utulivu; na kicheko kila mara. Sikumwona hata siku moja kama anahangaika. Anaangalia watu wote na matukio yote na macho ya mapendo, bila kukaza ngambo mbaya".

Kiisha miaka 5 ya naziri ya muda, Luigi anakubaliwa kwa naziri ya milele siku 5 Novemba 1959. Katika barua kwa wazazi Luigi anamshukuru Mungu.

"Hatua hiyo nilifanya na furaha, kwa maisha yangu yote, kwa milele. Nawasihi, mnisaidie kumshukuru Mungu sababu ya ibada hiyo inayokuwa alama ya kama Mungu anayenipenda".

Katika majifunzo ya Teolojia, Luigi anajitayarisha kuwa Padri. Siku 15 Oktoba 1961 Luigi anapata Upadirisho

Mwezi mmoja mbele ya Upadirisho Luigi anaonyesha furaha yake, akiwaandikia wazazi.

"Wapenzi wangu, sina neno la kuongeza, ila kusema kama nafurahi sana kabisa. Katika utulivu wa chumba changu, katika utulivu wa mchana wangu, naweza kuonja utamu wa zawadi Mungu aliyonipatia. Mfurahi nyinyi wote, wewe baba, wewe mama, ninyi wandugu na wadada wote; mkumbuke kama kuishi pamoja na Bwana ni tendo tamu kabisa; hivi tu tunatambua samani (valeur) maisha. Kila siku nawabeba pamoja nami katika altare ya Bwana. Mungu angeweza kuwa mwema zaidi?"



P. Luigi anapata habari ya kama anatumwa katika Misioni ya Congo. Furaha yake ni kubwa sana. Anawaandikia wazazi hivi:

> "Wapenzi wangu wote, mfurahi na mshangilie pamoja nami, kwa sababu nina habari njema na zawadi ya kuwapasha. Congo inaningoja. Mwaka 1961 ni mwaka wa Upadirisho wangu; mwaka 1962 ni mwaka wa Misioni yangu. Naitwa kutipula shamba la mizabibu la Bwana, naitwa kutumika katika shamba nzuri sana, shamba la matumaini, shamba la mahitaji. Matumaini makubwa ya kikristu yangoja Congo. Naitwa saa hii ya ajabu, ndiyo sababu siwezi kukosa usabiti na kumtukuza Mungu kwa moyo wangu wote. Ninyi pia mnisaidie kumshukuru Mungu. Hii ndiyo habari njema ya mwaka mpya. Nasema tena, furahini pamoja nami. Furaha ilitomboka jana, mwisho wa mwaka, wakati Padri Mkubwa, kwa rafla alitupasha ile habari. Nafurahi sababu mnafurahi, lakini nitakuwa na furaha kubwa zaidi kama ninaweza kuwasharikisha furaha yangu. Wengi wananiambia "Heri yako", lakini "heri yangu" mingi zaidi zinatoka moyoni mwangu".

Tukisoma maneno haya, hatuwezi kusahau barua ya Papa Francesco "Furaha ya Enjili". Mbele ya kuanza safari ya kuenda kwa Misioni anawaandikia tena wazazi:

> "Wapenzi wangu, baba na mama. Leo asubui nilinunua vitu vya lazima. Nilinunua chandaruwa(kwa kujikinga na mbu). Sasa tupo tayari kwa safari. Leo nilisoma Misa kwa ajili yenu. Kesho, kiisha misa, saa 11h49 tutakamata gari ya moshi mpaka Roma; tutafika 19h. Bwana atawapatia tuzo sababu ya majitoleo yenu ya ukarimu sana. Waliniambia ya kama 25.000 Banyarwanda, kiisha kufukuzwa (kutoka Rwanda) walingia katika Misioni yetu, na Askofu anatungoja sisi; hakuna mwengine wa kutumwa. Tuna usabiti sana sababu tunapendelewa. Wapenzi, utulivu na furaha vinajaa moyo wangu; ninyi pia muwe na furaha. Asubui, wakati nasoma Misa, mtie katika kikombe changu majitoleo na magumu yenu. Nashukuru watu wa mjini wetu, kwa sababu ya ukarimu wao; bila kufanya kitu nilipokea franka mingi. Nawakumbatia na nawabarikia wote".

Padri Luigi, kiisha kutembea katika Missioni ingine kwa kujifunza hali ya watu wa Congo, anatumwa katika Misioni ya Baraka. Luigi anaanza kutambua hali ya watu wa Baraka: watu ni watu wenye kumcha Mungu, lakini mara mingi wanachangachanga mambo ya kikristu na mambo ya kipagani.

Mapadri wa Baraka wanaangalia pia Misioni ya Fizi; mapadri wanapoenda Fizi wanakaa katika nyumba ndogo ya mbao, iliyojengua Uvira; nyumba ina viumba vinne. Padri Luigi anaona kama pa Fizi kuna wapagani wengi, Waislamu na Waprotestanti; shamba la Mungu kwa kupanda mbegu ni kubwa sana; inafaa kupanda mbegu, mavuno itakuja.

Siku moja P. Luigi anatengeneza kabumbu mbili iliyoharibika; hivi siku ya Mungu na kila siku mangaribi watu wanakuja kwa kucheza na kurafikiana na Mapadri. Padri Luigi anawaza juu ya Banyarwanda wanaokaa mbali na Misioni ya Fizi, juu ya milima. Askofu Catarzi anawapatia Mapadri wa Fizi kazi nguvu: kujenga nyumba mpya, sababu nyumba ya mbao ni ndogo.

Siku 11 Februari 1964 Luigi aliwaandikia wazazi wake barua; katika barua hii tuona kazi ya kitume ya misionari mpya, mshujaa na mfurahivu.

## Matengeneo

Siku ya Mungu mangaribi, nangoja watu watakaonisaidia katika safari ya kuenda milimani kwa Banyarwanda. Wanafika: ni vijana tano na mtoto mmoja. Mchana mzima walitembea na miguu, wanachoka sana, lakini wanafurahi sababu wanafika. Ni mara ya kwanza ya kuwaona, haraka tunakuwa marafiki. Tuliwatayarishia chakula kidogo; wanakula, wanapokea Sakramenta ya maungamo, mbele ya wengine wote, kiisha nawatuma waende kulala. Nawaambia "Mlale vizuri mpaka saa kumi na mbili (6h); kiisha tutaondoka".

## 27 Yanuari

Asubui na mapema naamka, nasoma Misa; natayarisha sanduku ya safari, nakamata kaawa, naamsha vijana wangu wanaokoroma bado; pa

6h tupo njiani kwa kuanza safari. Vijana wangu ni Banyarwanda, miguu mirefu, wanazoea sana kutembea. Kilometri saba ya kwanza ni sawa sawa, bila vilima, kiisha tunaanza kupanda; barabara haiko tena, njia ndogo inaanza. Vijana wangu wanafuatana katika mstari, kila mmoja na sanduku yake kichwani; mayani yanatufunika mara mbili, tena yanaingia katika njia yetu; sababu ya umande wa usiku, tunaloana mpaka nywele. Kiisha saa nne ya safari, kijana wangu mmoja anachoka sana, anatia chini sanduku, anakaa kwa kupunzika kidogo. Tunaomba kidogo ya "tokwa", mama mmoja ananipatia kidogo ya muwa. Natuma yote kwa kijana wangu aliyebakia nyuma sababu ya mchoko, il apate nguvu ya kuendelea. Tunafika kwa mto mdogo; pahali pa kutosha vyatu na kuchelewa, naruka juu ya mabega ya kijana wangu mmoja: tunavuka pamoja. Tunafika katika mto ndogo wa pili; navuka tena juu ya mabega ya kijana mmoja. Pa saa nne ya asubui tunakauka vizuri na jua, kama vile umande haingekuwa. Pa saa nane tupo miguuni mwa mlima mwengine.Tunapumzika, tunangoja wanaochelewa, kiisha tunakaza kupanda tena. Katikati ya mlima nachoka sana, nakaa, najilaza chini kwa kupumzika kido. Najipatia moyo, naendelea katika safari. Katika kilele cha mlima nakaa tena, tunatulizana; kwa leo hakuna milima tena. Sababu ya kukosa mazoezi niliwaza kama sitaweza kupanda milima, lakini nilishinda. Wananiletea maziwa ya ngombe; nakunywa; napata nguvu, napita mbele ya vijana wangu. Mvula ilinyesha tena muda wa nusu saa, kiisha jua kati inatukausha haraka. Mvula kabambi inakaribia: tunapiga mbio, tunaingia ndani ya kibanda: tunaisha fika salama. Protestanti mmoja anashangaa juu ya safari yetu sisi Mapadri, kwa miguu kwa kutembelea watu.

## Mapokeo katika mji mmoja

Tunafika katika mji mmoja; hapa tutalala usiku. Kundi moja ya watu walikuwa pale kwa kutungoja; waliponiona walipasha habari ya ujio wetu. Watu wote, wababa, wamama, watoto, wote wanafika kutusalimia na kunipatia mkono. Wote wanafurahi, sababu Padri anafika. Matembezi ya mwisho ya Padri, hapa, yalikuwa mwaka uliopita. Usiku unaanza kuingia; ukungu na upepo baridi vinatushauria kuingia ndani ya nyumba. Padri mwenzangu, mbele ya kuondoka, aliniambia: "Utafika na mchoko mingi. Usiungamishe". Lakini namna gani ningeweza kukataa?. Wakatekista wamoja na wakristu wa mji

waliniambia: “Padri, utuungamishe sasa, kesho watu watakuwa wengi, watatoka ngambo zote, hatutakuwa na wakati”.

## Hakuna wakati kwa kupumzika

Halafu nilifungua mlango na, bila kubadirisha manguo yanayochafuliwa na jasho, nilikaa katika kiti ndogo; waamini magoti chini; naanza kuungamisha. Bahati yangu, hawakuwa wengi; pa 18h30 wananiacha na wanaenda kula; natokotesha maziwa, nakunywa. Nilingetamani kusali Breviario na Rosaryo, na kiisha kujitupa katika kitanda; usingizi ungefika haraka. Pa saa 20h wanapiga hodi, ni wajirani, wanapenda kuongea na Padri. Basi, nasimama, nawapokea. Pa saa 21h30 wananiacha, natimiza mapashwa yangu ya kusali, naenda kulala. Nje ya nyumba, chini ya nyota ya mbingu, kundi la ngombe pamoja na walinzi wao: mbwa kubwa mbili wanalala karibu na mlango wa nyumba yangu. Naweza kulala bila masito.

## 28 Yanuari

Asubui na mapema jogoo anawika, lakini sisikii; sauti ya watu wanaokusanyika karibu na kibanda changu inanionyesha kama ni saa ya kuamka. Kibanda changu ni kubwa na refu; ina vyumba vitatu, moja kwa kujitayarishia chakula na kwa kulala, moja kwa kuongea na watu, moja inabakia wazi; siko mfalme, sihitaji vyumba vingi. Naamka, natoka nje, nawasalimia wote, tunaenda kanisani. Ni 7h; naungamisha mpaka 12h. Naanza Misa, yapata wakristu 80 wanakomunika; wanaimba na sauti kubwa nyimbo ya kinyirwanda.

## Padri Luigi anapita katika vijiji kwa kusikiliza watu

Wanaimba na furaha na juhudi; nyimbo zao zinistusha moyo wangu na moyo wa Bwana. Siwezi kufasiria, lakini nyimbo zinapenya moyo wangu, mpaka kulia machozi. Kanisa ni ya matope na paa ya majani, lakini Bwana anafurahi kukaa pamoja na watu wa milima, katika nyumba maskini. Kiisha Misa napunzika muda wa saa moja, nakula nacheza na vijana. Naanza tena kazi: nafanya mapepeto ya Wakatekumeni watakaobatizwa kiisha Paska; kujibu kwa maulizo. Usiku narudia nyumbani, nawasha taa ya petroli kwa kuendelea katika kazi. Pa 19h, nachamusha chakula, naanza kuonja, wanapiga hodi; ni vijana wawili ao watatu, wanasema kama Mkatekista aliwatuma kwa kuongea nami; walisema uwongo kwa kuingia kwangu; Mkatekista

hakuwatuma; hamu ya kuongea iliwasukuma kusema uwongo; vijana wengine wanakuja, pamoja na Wakatekista; maulizo mengi, majibu mengi ya kucheka mingi. Banyarwanda wanavuta moshi na kiko; kiisha kusalimiana wanapitishana kiko, kama vile alama ya undugu. Pa 22h wananiacha: nakuka chakula kidogo kilichogeuka baridi, nasali, kiisha najitupa katika kitanda changu ya ngumu na rafiki kila mara.

### 29 Yanuari

Kesho yake 7h maungamo ya wakristu waliofanya saa tatu ao nne kwa kuona Padri na kupokea Sakramenta. Misa nje ya kanisa sababu watu ni wengi: nakomunisha watu 130. Kiisha Misa Ubatizo wa watoto wachanga 25; natia katika kinywa cha watoto chumvi ya kutosha, watoto wanalambula chumvi na wanacheka. Imani ya wandugu hawa ni kubwa sana: wamama na watoto mabegani, wazee wanaotembea na mti; mama mmoja, chopi, mkatekumeni, alitoka mbali sana, na mti wake, kwa mapepeto ili akubaliwe kwa Ubatizo. Sawa na kondoo bila Mchungaji.

### 30 Yanuari

Nilikuwa na nia ya kuondoka asubui na mapema kwa kutembelea wakristu wa mji mmoja mbali sana, lakini wakristu wamoja walifika jana mangaribi, wanatamani Maungamo na Misa; nabadirisha mpango; siwezi kuwaacha bila Maungamo na Misa; nitaondoka kiisha 11h30; wananisindikiza wakatekista wangu watatu. Mitelemko na mipando, tunatembea mpaka 15h, bila kukuta hata mji mmoja. Mchana tulivu, mashamba yanayoja majani mabichi, mpaka mbali kwa macho, sawa sawa. Tunapanda mlima na namwuliza mkatekista: "mji wako uko wapi?"; na kidole ananionyesha "kule"; nasema tena: "tunapashwa kutembea mpaka kesho mangaribi kwa kufika kule?"; ananijibu: "hapana, Padri, sisi na saa tano ya safari tunafika kule". Hewa nzuri inabadirika, kungukungu na mvula. Pa 16h tunafika katika mji wa kwanza; wote wananirukia, wananiamkia kwa furaha, wakatolika, waprotestanti na wapagani; wananiomba nibakie pamoja nao usiku huo; waprotestanti wako wanajenga kanisa yao, wananiomba niibarikie; ni ya ajabu: protestanti anaomba baraka ya wakatolika. Vijana na wazee hawajaona bado Padri katika mji wao. Hata mara moja Mapadri walitembea katika njia hizo, kwa kutembelea vijiji vya hapa. Napita katika mashangilio, wote wananifuata, wananisindikiza kidogo,

wanaume, wanawake pamoja na watoto wao mabegani. Inanyesha, nasimama, kiisha naendelea, mwisho, pa 17h nafika. Natembelea wakristu wawili waliogeuka tena wapagani; nabakia pamoja nao saa moja; wananiomba maungamo; wandugu wawili wanarudia katika nyumba ya Baba; tulipe bei gani kwa kushukuru? Mvula kubwa kwa kurudia, bila koti na bila nguo ya kubadirisha; nakaa karibu na mto, na moto unanikausha. Usiku unaingia; kibanda kinajaa na watu; tunaongea mpaka 23h, kiisha, kama desturi.

### 31 Yanuari

Tunaanza na Misa, kiisha tunaondoka; wote wananisindikiza; watu wanaacha mji; hata waprotestanti wananikaribisha na kunisindikiza njiani, kwa muda wa kutosha; tunafuata njia ndefu zaidi kwa kumtembelea mkatekista aliyependa kuniona. Tunapita katika mji na miji na tunatembea tangu 10h30, mpaka 19h. Naanza kuzoea; wakristu walitembea muda wa saa tatu kwa kufuata Misa yangu ya leo; watafanya tena saa tatu kwa kufuata Misa ya mwisho, kesho.

### 1 Februari

Misa ya mwisho katika milima kwa ajili ya Banyarwanda. Pa 10h30 tunaanza safari na juhudi sana, tusilale tena njiani; pa 18h tunafika Lubondja.

### 2-3 Februari

Misa pa Lubondja; mangaribi wanafika P. Giovanni Didonè na Askofu. Pamoja nao tunarudia Fizi."

**Padri Luigi hakujifunza Teolojia ya "Ekumenismo", maana yake namna ya kuongea na wandugu waprotestanti, lakini aliishi kindugu na wakristu Waprotestanti, sababu ya imani moja kwa Yesu Kristu; ndiyo ekumenismo ya undugu na ya mapendo, mbalimbali na Teolojia ya Ekumenismo. Kadiri alivyosema P. Amato Dagnino aliyeishi na P. Luigi pa Baraka, kwa wakati fupi:**

"Padri Luigi alikuwa anapenda sana kutenda kuliko kusema".

**Safari kwa kuwatembelea wakristu inamletea Padri Luigi furaha kubwa, japo magumu ya njia, ya mvula na baridi:**

> "Watu wanatupenda sana, wanatusaidia; wote walinipatia chakula: maziwa, mayayi na kuku mbili. Safari ni ya magumu, lakini tunaifanya na mapenzi mema; nasikia huzuni sababu sikuweza kuondoka leo tena pamoja na Padri Didonè".

Mwezi mmoja mbele ya kuuawa, siku 22 Oktoba, Luigi anaandika hivi kwa wazazi na wandugu:

> "Wapenzi wangu, mama, baba, wandugu, wadada: niko vizuri. Mungu alinikinga kwa namna ya ajabu: sikufungwa, sikupigwa. Tangu siku 16 ya Oktoba niko hapa Baraka kwa kukomboa mapadri wawili wanaokuwa Italia. Siko mimi peke yangu; yupo pamoja nami Frera Faccin. Mbele nilikuwa nikifanya safari Fizi-Baraka, Baraka-Fizi; sasa ni magumu kwenda huku na huku. Sasa nakaa hapa Baraka. Tunaweza kufanya kazi kidogo kidogo: nyumba, kanisa".

Katika barua yake ya mwisho kwa wazazi, siku 22 Novemba 1964, siku sita mbele ya kutoa uzima wake kwa Enjili ya Yesu Kristu, P. Luigi anaandika hivi:

> "Waprotestanti waliisha enda tangu zamani; sisi tunabakia. Ni hatari. Mnikumbuke mbele ya Bwana pamoja na wenzangu wanne tunaokuwa katika hali moja. Nawakumbuka mara mingi.
>
> Nawakumbatia wote katika Bwana, hasa baba na mama. Tupo mikononi mwa Mungu. Mtuombee na mwaambie watu watuombee. Chakula hakikosi, amani ndiyo inakosa. Wengi wako juu ya Kalvaryo".



# SEHEMU YA NNE: PADRI GIOVANNI DIDONÈ

“Ni mashahidi wenu;
mwandike historia yao;
mheshimu maiti yao”.

Ndiyo maneno ya Mtakatifu Paulo VI, kwa Askofu wa Uvira Danilo Catarzi, wakati alimwambia papa kama wandugu wanne waliuawa kwa aji ya Kristu, katika Congo. Tukisoma historia ya mashahidi ya Enjili katika Congo, mwaka 1964, tunakumbuka “Historia ya Mashahidi ya Yesu Kristu”, mwanzo wa Eklezya. Kifo cha Padri Didonè hakikuwa msiba wa rafla, ila kilele ya maisha yote ya mtu anayejitolea kila siku kwa Yesu Kristu.

Padri Luigi Menegazzo, Padri Mkubwa wa Xaveriano wote, anaonyesha fazila ya Padri Didonè.

“Historia ya mashahidi wetu xaveriano inahamusha ndani mwetu: uhodari, utulivu, shukrani kwa Mungu, ombi kwa Roho Mtakatifu ili jamaa yetu ya wamisionari iwe na utii na uhodari katika utumishi wa kutangaza Enjili. Mshahidi si mshujaa tusioweza kuiga, ila ni mfuasi wa Yesu, anayeishi na uaminifu na utulivu wito wake, asiyekubali kuvutwa na miungu mengine, anayekaza macho katika Kristu.

Didonè hakusita, hakurudia nyuma. Karisma xaveriano ilikuwa njia yake: kujitolea kwa Kristu na kwa Enjili, katika mambo yote na kwa maisha yote, kujikatalia wenyewe ili Kristu atawale katika maisha yetu ya utii, umaskini na usafi wa moyo, kwa kufanana zaidi na zaidi na Kristu. Kuungana na Kristu, kuishi na Yeye, ndiyo karisma ya Waxaveriano”.

Giovanni alizaliwa katika mji wa Rosà (Vicenza), siku 18 Marsi 1930; wazazi wake Angelo Didonè na Maria Marchetti. Ndoa ya Angelo na Maria ilibarikiwa kweli na Mungu: walizaa watoto kumi na moja; saba kati yao walijitolea kwa Mungu, kama vile Mapadri ao Masera.

1. Paolina: bikira wa "San Comillo de Lellis"; aliisha kufa.
2. Giovanna: bikira wa "Figlie di San Giuseppe"; anatumika katika Italia.
3. Domenico: alfunga ndoa na Celestina Cecchin; walizaa watoto watatu.
4. Giovanni: Misionari Xaveriano, Mshahidi wa Yesu Kristu.
5. Teresa: aliolewa na Alberto Fabris; walizaa watoto watatu.
6. Luigi: alioa Domenica; walizaa watoto watatu.
7. Severino: aliingia katika jamaa ya "Don Orione"; anatumika katika Italia.
8. Amabile: aliingia katika jamaa ya "Missionarie di Maria-Saveriane"; anatumika katika Brasile.
9. Agnese: aliingia katika "Suore Dorotee di Giovanni Farina": alitumika katika Colombia, sasa katika Italia.
10. Camillo alizaliwa mwaka 1941, ni Misionari Xaveriano; anatumika katika Brasile.
11. Albino; alijaribu kuwa Misionari Xaveriano, mwisho alioa Maria Menghetti.

Wazazi wa Giovanni Didonè walikufa katika Bwana: Baba Angelo siku 13 Augusti 1971, mama yake siku 21 Septemba 1973.

Giovanni alipenda sana wandugu na wadada zake, lakini mpendelevu wake alikuwa Severino ya jamaa ya "Don Orione".

Giovanni alihuzuria naziri ya Severino na furaha kubwa na aliandika kwa dada yake Paolina:

> "Severino kweli ni mkubwa; niko hakika kama katika utakatifu anatupita wote. Nilimwona nyuma ya kutoa naziri, alilia machozi, nilimwona, alikuwa na furaha na mushangao. Pamoja na Severino mimi pia nililia machozi; niliwaza: Mungu alitupenda na anaendelea

kutupenda, alipenda sana jamaa yetu, hapo na moyo unaojaa shukrani, niliimba "Moyo wangu unamsifu Bwana".

Baba yake Angelo angetamani mtoto wake Giovanni awe Padri wa Diosezi ya Vicenza kwa kuweza kubakia pamoja naye. Ndiyo sababu Giovanni, muda wa miaka mitatu (1947-1950) alijifunza katika Seminario ya Thiene (Diosezi ya Padoue). Lakini nia ya Giovanni ilikuwa kugeuka kuwa Misionari Xaveriano. Baba Angelo katika machozi alimwambia Giovanni:

"Nilidanganyika…. kukuondosha kwa wazo hilo.
Lakini fuata njia yako".

Hapo Giovanni aliomba kukubaliwa katika jamaa ya "Missionari Saveriani"; alikubaliwa na alingia katika Noviziati ya "San Pietro in Vincoli" siku 11 Octoba 1950.



Giovanni katika mwaka wa Noviziati alijifunza picha ya Misionari Xaveriano aliyofanya Mtakatifu Guido Maria Conforti:

> "Misionari ni mtu anayejitolea kuishi maisha mazuri ya utakatifu; alimtazama Yesu Kristu anayeonyesha kwa mitume dunia kwa kuishinda na Enjili, siyo kwa bunduki, ila kwa mapendo na moyo mwema. Misionari anavutwa na Kristu, ndiyo sababu anaacha jamaa, nchi na marafiki wote. Silaha yake ni Msulubiwa, kila mara tayari kutoa damu yake kwa ajili ya wandugu. Misionari anapashwa kuwa picha ya Yesu Kristu, kila mara anatenda kadiri alivyotenda Yeye; mara na mara anajiuliza: katika matukio ya leo Yesu angetenda nini, angetenda namna gani?"

Mwisho wa Noviziati Didonè anaomba kukubaliwa katika jamaa ya "Missionari Saveriani", akisema kama "Najua nafanya nini, najitolea kwa furaha". Siku 12 Octoba 1951 katika "San Pietro in vincoli" anatoa naziri ya utii, umaskini, usafi wa moyo na kujitoleaa kwa kutangaza Enjili.

Kiisha naziri Giovanni anaenda Desio kwa majifunzo ya filosofia. Karisma ya Waxaveriano ya kuungana na Kristu inaingia katika akili na moyo na inafasiriwa na maneno ya Giovanni. Katika barua kwa dada yake Tecla:

> "Tukaze macho kwa Yesu. Ni Yeye Yesu anayewapatia mashahidi, na sisi pia, nguvu na uhodari. Tumwamini Yesu na tukomae katika mapendo yake; hatuwezi kuogopa mambo yatakayokuja. Kama mapendo ya Yesu yaongezeka, tunavutwa kufanana naye. Wakati mtu anatambua katika wagonjwa Yesu, na anawasaidia kama vile wangekuwa Yesu, imani yake ni kubwa, imani ya watakatifu. Nawaza kama ni ya lazima kuwa na imani kubwa zaidi kwa kumtambua Yesu katika wagonjwa, kuliko imani kwa kumtambua katika Ukaristia".

Katika barua ngine kwa dada yake Tecla, Giovanni anashauria ibada kwa Bikira Maria:

> "Kujitolea kwa Bikira Maria ni kitu kizuri sana; siku kwa siku najisikia kama naamini zaidi, naishi katika utulivu zaidi, bila kuogopa mambo yatakayokuja. Najiweka mikononi mwa Bikira Maria, sababu niko wake, nasikia amani kubwa na furaha."

Siku kuu ya kupata Upadirisho inakaribia; Giovanni anaandika barua kwa P. Giacomo Spagnolo, Msimamizi ya Teolojia ya Waxaveriano. P. Spagnolo anamshuhudia:

> "Giovanni anapenda sana kuwa Padri; mawazo yake na huba yake mara mingi ni Upadirisho."

Siku chache mbele ya Upadrisho, akimwandikia Mama Parolin, anaonyesha furaha yake:

> "Najitayarisha kwa ile siku kuu, karibu sana. Naona kama ni ndoto: niliisha fikia ukomo niliyotamani sana. Nasikia ndani mwangu furaha kubwa na utulivu, msukosuko na matumaini bila kipimo. Uniombee ili nipande altare ya Bwana na moyo unaoshtahili. Nikifiri juu ya ile siku, nalia machozi ya furaha".

Siku anayotamani sana inakuja; siku 9 Novembe Giovanni anageuka kuwa Padri.

Siku ya Misa yake ya kwanza Giovanni aliomba zawadi tano:

- Kwa Mungu Baba: kubakia mwaminifu mpaka mwisho ya maisha yake.
- Kwa Mungu Mwana: mapendo makubwa kwa Bikira Maria.
- Kwa Roho Mtakatifu: ushuhuda wa kifo kwa ajili ya Yesu.
- Kwa Bikira Maria: usafi wa moyo, sawa na wamalaika.
- Kwa Fransisko Xaveri: juhudi katika kazi ya kitume.

Kiisha kupata Upadirisho Giovanni anaendelea kujifunza Teolojia pa Parma, muda wa mwaka mzima 1959; kiisha anatumwa Ubeleji kwa kujifunza kifranza, sababu alichaguliwa kuwa Misionari katika Congo.

Siku kuu ya Mtakatifu Fransisko Xaveri, 3 Desemba, Giovanni anaacha Italia kwa kuenda Congo na masangao na furaha kubwa. Misioni iliyochaguliwa kwa ajili ya Giovanni ilikuwa Baraka, 90 kilometri na Uvira, pwani pa ziwa Tanganika. Giovanni alifanya safari yake ya kwanza ya kitume, na “Père Blanc” mmoja, Padri Mkubwa wa Misioni ya Baraka. Safari ilidumu mwezi mmoja, tangu 9.2.1960 mpaka 9.3.1960, na miguu, kupanda milima na kuishuka. Katika ile safari Padri Mkubwa alibatiza watu 185; P. Giovanni alibatiza 40 watoto; waliacha 30 wakatekumeni wapya.

Kiisha Padri Giovanni anaenda Fizi.

Katika barua aliyomwandikia ndugu yake Severino, anafasiria kazi anayofanya; safari na gari, kuzama katika potopoto, wanamwomba franka kwa kusukuma gari; wengine wanaisukuma kwa mapendo, bila kuomba kitu; wakristu wanamgoja kwa maungamo na komunyo; kufanya mapepeto ya wakatekumeni wapate kuendelea katika vyeti vya II, III, IV; mpako wa wagonjwa kwa wagonjwa wamoja; mchoko wa safari na homa ya Padri; kulala na blanketi mbili au tatu juu ya milima. Kutayarisha wakatekumeni kwa Ubatizo (Kasompe) inakamata juma mbili na kila siku mafundisho mawili; kutembelea 200 wakoma katika mji wao; kutayarisha mawe kwa kujenga kanisa; kukusanyisha vijana kwa njia ya kabumbu.

Padri Giovanni anaacha Baraka na anafika kiliba, katika mipaka na Burundi. Katika Bujumbura wanafika wakomunista wa nchi mbalimbali: Rusia, China, Cuba, Afrique du Sud. Hawa wote wako tayari kuingia katika Congo, kuwasha moto wa vita, kuiba madini ya Congo na kuleta komunismo inayokana Mungu.

Padri Giovanni anarudia tena pamoja na P. Vagni na frera Faccin, Baraka. Halafu wanalazimishwa kupanda mpaka Fizi; wanafika kiisha usiku kati; wanafungwa gerezani; kesho yake wanaruhusiwa kutelemuka Baraka na kurudia Kiliba. Tupo mu mwezi wa tatu 1961. Masera wa Kiliba walipashwa kukimbia Bujumbura, Padri Giovanni alirudia Fizi na alibakia Fizi mpaka siku ya kufa kwake. Alipata magumu mengi, alizarauliwa na wamulele; yeye alivumilia yote na moyo hodari; watu walimshauria akimbie katika Urega, lakini yeye aliwajibia kila mara kama hawezi kuacha ndugu zake.

Siku mmoja wanamwambia Frera Pirani, "pilote" ya "petit porteur" yetu: "Ee bwana frera, umwambie Askofu amwondoshe Padri huyu, kutoka Fizi; kama si vile tutamwua".

Siku ingine Wamulele wanakuja, wanakamata Padri Giovanni na Mpishi wa nyumba, wanawapeleka mbele ya kanisa, wanawafunga mikono nyuma ya mabega, wanawazarau, wakati jua ilikuwa kivukutu kali. Padri Giovanni hakusema kitu, alivumilia tu. Siku ngine Padri Giovani alipelekwa nyuma ya chumba cha kulia, alivuliwa nguo, alifungwa na kupigwa makofi.

Siku 9 Novemba 1964 (iliisha pita miaka sita tangu alipata Upadirisho), siku 19 mbele ya kufa kwake, Padri Giovanni anamwandikia Mkatekista Raphael Papu:

> "Msimame wima, nawasihi. Msikate kitumaini. Mungu yupo. Mapadri pahali pa kukimbia, wanapenda zaidi kubakia na kufa. Tulitumwa ili tubakie hapa, Fizi.
>
> Msimame wima, msianguke. Msiache watoto kufa bila Ubatizo. Si lazima maji ya baraka; mwabatize na maji ya kawaida. Wanaopenda kufunga ndoa wangoje kidogo".

# SEHEMU YA TANO: ABBÉ ALBERT JOUBERT

Papa Mtakatifu Paulo wa VI, mwezi wa kumi na mmoja 1966, akiongea na Askofu wa Uvira Danilo Catarzi, kiisha kusikia habari ya kifo cha mashahidi wetu: Vittorio Faccin, Luigi Carrara, Giovanni Didonè na Albert Joubert, alimwambia:

“Ni Mashahidi wenu,
mwandike habari ya maisha yao.
Mheshimie maiti yao”.

Albert Joubert alikuwa mkongomani, padri wa Jimbo la Baudoinville, kisha Kasongo, mwisho ya Uvira; aliishi pamoja na wandugu wetu Waxaveriano, alisali pamoja nao, alikula pamoja nao, alimtumikia Mungu na watu pamoja nao, pamoja nao pia alikufa mshahidi wa Yesu Kristu.



Baudoinville (Kirungu) 06.10.1935: upadri wa abbé Joubert Albert

## Baba yake: Léopold Louis Joubert (1842-1927)

Léopold-Louis Joubert ndiye baba wa Albert. Léopold alizaliwa pa Saint Herblon siku 22 februari 1842, katika France; alipokuwa na miaka 18 alikuwa askari, na muda wa miaka 10 alikuwa mtumishi wa nchi Vaticano, wakati wa papa Mwenye heri Pio IX.

Alipokuwa na miaka 28 alifika Afrika kwa kukinga safari ya Wamisionari "Pères Blancs". Alikaa mjini mwa Mpala na alichaguliwa kuwa msimamizi wa jimbo ndogo Tanganika. Léopold alipenda Afrika, kama vile ndugu wa watu wa Afrika alipigana na "esclavagistes". Léopold alioa mwanamke wa Congo, Agnès Atakae; alizaa naye watoto kumi walioadibishwa katika imani ya kikristu; kati yao watoto wawili walipata Upadirisho na binti mmoja aligeuka kuwa bikira.

Léopold alitumika kama vile misionari mulaiki. Aliitwa na watu "askari mtakatifu"; alikuwa pia mkatekista na tena alifanya nguvu ili haki ya waana Congo iheshimiwe na wasiuzwe tena kama vile mbuzi. Padri Mkongomani Kaoze Stefano alikuwa rafiki wa Léopold Joubert na wa jamaa yake. Miezi michache nyuma ya kifo cha dada yake aliyeuzwa kwa "eslavagistes", Kaoze pia anafungwa kwa kuuzwa. Wezi wa Kaoze, njiani wanakutana na watu wa "capitaine Joubert"; wanaacha uhuru mtoto na wanakimbia. Musa mpya wa Afrika anakombolewa.

Kiisha kufa kwa Léopold siku 27 Mai 1927, Padri Mkongomani Kimembe aliandika maneno haya juu yake:

> "Capitaine Joubert alileta amani katika nchi yetu, alifukuza Waarabu. Alipooa kikristu binti wa kwetu, alituonyesha heshima na mapendo. Alipigana na desturi ya ulozi na hivi alipunguza mateso ya watu wengi na kuwapatia moyo. Mapendo yake yalionekana hasa katika kazi ya kutunza wagonjwa na kuwasaidia maskini. Aliwatolea watoto wake wawili kwa kazi ya Padri. Tunamwita: mfalme wa kweli wa nchi, baba wa watu weusi, mtakatifu".

Baba Léopold alitimiza utumishi wa Vatikano wa II kwa ajili ya walaiki: kutangaza Enjili na kumshuhudia Kristu.

## Agnès Atakae, mama wa Albert (1874-1958)

Padri Stefano Kahoze, padri wa kwanza wa Congo na rafiki ya jamaa Joubert, aliandika maneno hayo juu ya Agnès, mama wa Albert:

> "Agnès Atakae alirisi kwa wazazi wake tabia ya amani na ya heri, pamoja na utii mzuri. Alikuwa binti mnyenyekevu, mpenda usafi wa moyo, kama vile wananawake wa milima ya Marungu. Japo alikuwa bibi wa mkubwa, hakuonyesha cheo chake, hakujisifu na kiburi, ila alikuwa mpole na mnyenyekevu, akivaa nguo ya kawaida. Wakati alichaguliwa kwa kuongoza wabinti wenzake kwa kazi ndogo, alitumika na hekima, mapendo na furaha. Katika michezo aliwafurahisha wote. Pamoja na bwana wake alikuwa akipenda sana maskini na kuwasaidia".

Perpetua, masera wa jamaa ya "Mtakatifu Yosefu wa Moba", aliandika maneno haya juu ya Agnès Atakae, mama wa Albert:

> "Agnès, mama wa Padri Albert, alikuwa na moyo mkarimu kwa ajili ya wamaskini. Yeye aliwapokea na kuwatunza, kama vile watoto wake. Aliwapokea katika nyumba yake watoto na watu wazima na kuwatayarishia chakula; kazi yake ilikuwa: kuwakusanyisha watu na kuwapokea".



Mpala, 13.02.1888: Ndoa ya capitaine Joubert pamoja na Atakae

Albert alizaliwa mjini mwa “Saint Louis de Mrumbi” siku 21 Novembe 1908; kesho yake alibatizwa. Alipokuwa na miaka 6 alikomunika, na miaka 7 alisabitishwa. Alipokuwa na miaka 12 Albert aliingia katika Seminario ndogo, katika mji wa Lusaka, 50 Kms mbali na Baudoinville (Kalemie). Wakati huo (1920) Papa Benoit XV alitaja wenye heri mashahidi wa Uganda: tendo hilo ilipashwa kuwapatia waseminarista wa Congo huba kubwa ya kuwa Watakatifu.

Kiisha miaka tano ya majifunzo katika Seminario ya Lusaka, Albert anaandika barua kwa Askofu Roelens kwa kuweza kuingia katika Seminario kubwa. Barua hii, katika luga ya kifransa maskini, inaonyesha tabia ya Albert: unyofu, uwazi, unyenyekevu, mapenzi mema ya kutii kwa kugeuka kuwa padri mzuri. Wakubwa wa Seminario ndogo wanaandika ripoti juu ya Albert:

> “Albert Joubert: akili nzuri, uchunguzi mzuri. Tabia: mwenye kujichukiza, mwenye kiburi. Fazila: anapenda musiki na kazi ya mikono, mtu wa ibada, adabu nzuri, anazoea kujitolea, anapenda usafi na usawa. Albert anapashwa kujikaza ili tabia yake iwe nzuri zaidi”.

Albert anakubaliwa katika Seminario Kubwa; alikuwa na miaka kumi na saba. Albert anajitayarisha katika Seminario kubwa ya Baudoinville kwa kuwa Padri (1925-1935).

Albert alifuata miaka tatu ya Filosofia na miaka 6 ya Teologia. Maisha katika Seminario kubwa inafuata mpango wa kawaida: kujifunza, kusali, kazi ya mikono, “sport”, matembezi. Albert anaendelea kuzoea kuishi na wenzake namna ya kindugu. Zaidi ya majifunzo ya Filosofia na Teolojia, Albert anafanya mwaka mmoja katika Seminario ndogo ya Lusaka (1934): anawafundisha Waseminarista wadogo kilatini. Ushuhuda wa Mapadri, kiisha mwaka huo mzuri, Albert anakubaliwa kurudia katika Seminario kubwa kwa kujitayarisha kwa Upadirisho. Lakini ushuhuda unaonyesha kosa moja: kuchelewa kwa kufika kanisani kwa sala ya asubui.

Mbele ya Upadirisho Albert anatoa maagano yake:

> "Najua agano la usafi wa moyo ni nini. Najitolea kwa moyo wangu wote kuishi agano hilo na mapenzi mema, mpaka mwisho. Najitolea kutii kila mara. Niko tayari kutoa mifano mizuri katika maneno na katika matendo, kwa kupata neema kwa Bwana".

Siku 6.10.1935, katika Kanisa kubwa ya Mtakatifu Yosefu ya Baudoinville, Albert Joubert anageuka kuwa Padri kwa milele; yeye ni Padri wa 15 ya Vicariat Apostolique ya Baudoinville. Albert alifurahi sana pamoja na mama yake Agnès na ndugu zake (baba aliisha kufa 1927).



Mungombe 1961: Abbé Albert Joubert

Kiisha Misa ya kwanza mjini mwake, Padri Albert anatumwa Kasongo kwa kumsaidia Abbé Noel Mala atakayekuwa Askofu wa Kasongo mwaka 1963. Anatumika Kasongo muda wa miaka 2 katika “Chapelle-Ecole” (Nyumba ya Mungu na Masomo).

Pamoja na Wakatekista-Walimu, Albert anatangaza Neno la Mungu na anafundisha kusoma na kuandika. Kiisha miaka miwili ya utumishi wa Padri katika Kasongo, Albert anatumwa Kala (1937-41), misioni mbali na Kasongo Kilometri 600; siku kumi na tano kwa kufika Kala, misioni iliyoaminiwa kwa mapadri wakongomani peke yao. Padri Mkubwa wa Misioni alikuwa Padri Kaoze na Padri Albert alikuwa “mlinda hazina”. Abbé Kaoze, na furaha na shukrani kwa Mungu, anafasiria kazi wanayofanya Mapadri 4 (Kaoze, Albert, Kiabi, Kalombe).

Wakaaji wanafurahi na kazi ya Mapadri Wakongomani: wengi wanafika kwa Misa na kwa mafundisho; wakristu wa kizuio wanajitolea kwa namna ya kurudishiwa Sakramenta. Wakati wa kipwa wenye kufuata ukatekumeni na Misa wanaongezeka. Hesabu ya wakatekumeni inaongezeka kila mara. Kwa kusaidia kazi ya mapadri na maendeleo, watu wanalima shamba la mingazi na miti mbalimbali ya matunda. Wakristu wanajitolea kuleta mawe kwa kujenga kanisa npya ya Kala.

Albert, akifuata mifano ya wazazi wake, alikuwa mkarimu mbele ya wamaskini.

Siku moja Albert, akishikwa na huruma kwa ajili ya jamaa ya watoto 13 ya Kalonja, alimpatia binti kikapo kikubwa cha ulezi. Watu walisema mingi. Abbé Stefano Kaoze alimkaripia Albert. Albert anakubali kosa. Wengine wanasema:

> “Ni kosa gani? Abbé Kaoze, wewe ulifanya kosa; pahali pa kumkaripia Albert ungepashwa kumsifu na kumpatia moyo!”

Hapa tuona fazila mbili ya Albert; ukarimu kwa wamaskini, kuteswa kwa ajili yao katika kimya na unyenyekevu.

Kiisha miaka nne pa Kala, Albert anatumwa tena Lusaka, katika Seminario ndogo (1941-45), kwa kufundisha Waseminarista na kusaidia kazi ya kitume katika shirika ya mbali. Wakati huo Albert alijitolea katika safari ya kitume. Katika desturi ya

Misionari wa Afrika (Pères Blancs) mapadri wa misioni wanatembelea shirika za wakristu wa mbali, muda wa juma au mwezi moja. Kazi ya kufanya katika safari: kuungamisha wakristu wapate kuhuzuria Misa na kukomunika kila siku, kuwaongoza wakatekista na wakatekumeni, kutembelea wagonjwa; kufanya mapepeto ya watoto wa Komunyo ya kwanza na ya wakatekumeni; kuwaandikisha katika kitabu watu waliobatizwa katika hatari ya kufa; kuwasikilizisha na kuwapatanisha watu wenye na magomvi kati yao. Albert alijitolea katika utumishi unaofanyiwa katika safari.

Kiisha miaka nne katika Seminario ndogo ya Lusaka, Albert alitumwa Moyo (1945-53) kwa kuishi na kutumika pamoja na Misionari wa Afrika (Pères Blancs). Katika Misioni ya Moyo Albert alipewa kazi ya kuangalia na kuongoza masomo ya katolika, ili vijana waadibishwe na wakomae kikristu. Albert alizoea kuishi pamoja na mapadri, pa Kala pamoja na mapadri wakongomani, sasa hapa Moyo pamoja na Misionari wa Afrika (Pères Blancs) wanaoheshimia sana maisha ya shirika ya kindugu.

Mwaka 1952 "Vicariat Apostolique de Baudoinvile" inazaa "Vicariat Apostolique de Kasongo". Katika mpango huo mpya, mapadri wakongomani 5 wa Baudoinville wanaingia katika "Vicariat Apostolique de Kasongo": Bruno Kalumbwa, Ignace Kaumo, Thomas Maliyabwana, Albert Joubert na Pierre Lubeba. Tangu sasa Albert ni padri ya "Vicariat" ya Kasongo.

Mwaka 1953 Abbé Albert anaenda Kabambare(1953-1956). Wamisionari wa Afrika (Pères Blancs) wanaacha Kabambare na kuweka Misioni katika mikono ya Mapadri wakongomani. Albert anageuka kuwa Padri Mkubwa, anasaidiwa na mapadri Pierre Lubeba na Ignace Kaumo. Askofu wa Kasongo Cleire anawatumainia mapadri wakongomani na anafurahi sababu ya kazi yao katika Kabambare; hivi anaweza kuunda Misioni ya Kisamba, mtoto wa misioni ya Mingana, kwa kutangaza Enjili kwa Waislamu.

Mwaka 1956 Askofu Cleire anatembelea Misioni ya Kabambare na anairudisha katika mikono ya Wamisionari wa Afrika (Pères Blancs), akituma Mapadri wakongomani: Albert kwa Kibangula,

Kalumbwa kwa Kalima, Kaumo kwa Kasongo; wote watatu kwa kuongoza masomo.

Albert anatoka Kabambare kwa kuenda Kibangula (1956-1857) kwa kutumika pamoja na Wamisionari wa Afrika (Pères Blancs), kama vile msimamizi wa Masomo. Kama vile alivyozoea, Albert alishurulika na Masomo na kazi mbalimbali ya kitume. Katika Misioni ya Kibangula Albert pamoja na Wamisionari wengine walipata magumu mengi katika kazi ya kutangaza Enjili: watu wanaishi katika hali ya ulozi na chuki; vijana wengi wanaishi na wabibi zao bila Sakramenta ya ndoa, sababu ya kukosa mali ya kuoa (dot); wabinti wanalazimishwa kufuata dini ya wabwana wao. Wakati huo pa Kibangula Albert, kwa gari kubwa, anapeleka wanafunzi huko na huko na wagonjwa wa Lusangi.

Safari ya Albert haijamalizika; kwa mara ya pili anatumwa Moyo (1957-1958). Muda wa mwaka mmoja Albert aliishi na Wamisionari wa Afrika (Pères Blancs) akionja huzuni na furaha ya maisha ya kindugu pamoja na Mapadri wanaotoka Ulaya.

Askofu Cleire siku 27.8.1958 anasindikiza Albert mpaka Seminario ndogo ya Mungombe (1958-1963) apate kufundisha Waseminarista. Katika Semnario ya Mungombe Albert anakutana na Mapadri Xaveri (Pères Xavériens) na anaanza kutumika pamoja nao. Mwaka 1962 iliundwa Diosezi ya Uvira na Seminario ya Mungombe inaingia katika udongo wa Diosezi ya Uvira. Albert anaanza kuwa Padri wa Diosezi ya Uvira.

Padri mkongomani Charles Bilembo alimfahamu Albert Joubert na anatoa ushuhuda huo juu yake:

> "Fazila ya maisha ya kipadri ya Albert ilikuwa adabu na utii wake. Japo alikuwa mtoto wa Mkubwa mtajiri, kila mara alikuwa wazi na mnyofu; kila mara alijiona kama Padri wa Afrika. Albert hakuzarau hata mara moja watu weusi. Albert aliishi utii: kila mara alikuwa tayari kutii, wanapomtuma haizuru wapi. Hakutafuta upendeleo wala ruhusa."

# SEHEMU YA SITA: KIFO CHA MASHAHIDI WETU

Siku 24 Novemba 1964 jeshi nzima ya ”Armée Nationale” linafika Lulimba kwa kukamata Fizi na Baraka. Wamulele karibu elfu moja wanangoja njiani kwa kuwakamata katika mtego. Wabembe wa Baraka walifika kwa kuwasaidia Wamulele.

Mwongozi wa Simba alikuwa Abedi Masanga, mkaaji ya Katanga, mji mbali na Baraka km 9, katika njia ya Fizi. Abedi Masanga anaitwa pia Kibwa Amu Floribert; alikuwa na wabibi 3; bibi wa mwisho ni Maonyesho Musa. Abedi alikufa pa Masongela Nonda, mbali na Kasongo 50 Km, njia ya Lusangi, mwaka 1997. Mwanzo Abedi alikuwa msermala pa Baraka; kiisha aliingia katika kundi ya Wamulele; akajionyesha wazi kama mtu wa asira na ujeuri sana; aliunda kundi la waasi na yeye mwenyewe alijitaja “lieutenant, capitaine, commandant, colonnel”.

Siku 30 Yuni, pamoja na kundi lake alikuwa Nakiliza na yeye mwenyewe aliua mkubwa wa ”Frères Maristes”, akimshtaki kama vile “commando belge”. Abedi alizoea kuvuta bangi na kulewa na kanyanga. Mapambano kati ya ”Armée Nationale” na Wamulele yalikuwa makali. “Mercenaires” wanasaidia “Armée” na ”automitrailleuses, mortiers et armes automatiques”; ile siku walikufa 700 waasi. Hata wenzake wa kundi la Abedi walikufa wengi. Abedi anaona karibu yake maiti mingi, anashangaa, anabakia yeye peke.

Kesho yake, pamoja na kundi ndogo ya wale waliobakia wazima, anaacha Lubondja, anafika Fizi wakati wa kutua kwa jua. Hasira na ujeuri kwa Wamisionari unaongezeka katika moyo wa Abedi; anawaza kama kushindwa kwao pa Lulimba ni kosa ya Mapadri. Bila kukawia anaenda Fizi, kwa Mapadri, katika Missioni, kwa kuomba vinywaji; usiku mzima alifanya fujo kubwa mjini mwa Fizi. Abedi Masanga hakuwa mkristu; alikuwa na hasira kubwa kwa dini.

# Kipindi cha 22: Wandugu wetu wanne wanakufa kwa ajili ya Yesu

## *Frera Vittorio Faccin anauawa*

Kesho yake, ulevi wa ajabu ulimfanya Abedi kuwa mpoketevu (arrogant), tena na ujeuri mpaka kuwa mtu wa hatari hata kwa wenzake; kiisha anatelemuka Baraka na gari inayojaa wasimba. Saa tatu ya asubui gari ilisimama mbele ya nyumba ya Mapadri. Frera Facciin tangu saa moja alianza kazi; alikuwa ndani ya chumba cha kuongoza kazi, anasikia sauti ya wasimba wanaosimama mbele ya mlango; frera anatoka kwa kutuliza watu; wasimba saba ao nane wanamzunguka; Adedi alikuwa karibu na gari na anaanza kumkaripia frera sababu ya "Radio-phonie"; anaamuru frera apande na yeye katika gari; frera anaitika; gari inasimama mbele ya kanisa; frera anabakia peke yake katika gari; "colonnel" anamwambia frera kama pamoja naye wataenda Fizi; frera anajibu:

"Siwezi kuacha Padri peke yake hapa Baraka".

Ndiyo maneno ya mwisho ya frera; hapo anajaribu kufungua mlango wa gari kwa kutoka. Hata wasimba waliona kama ni mwisho, hapo wanajiweka mbele ya Abedi anayekuwa na bunduki mikononi (révolver) kwa kuua frera; Abedi katika hasira anaogopesha wenzake na bunduki; hapo hao wanajiweka pembeni; frera anasimama kwa kutoka kwa gari; risasi 3 zinafika kwa kifua cha frera, hata kutoboa bati (tòle) ya gari; frera Vittorio anaanguka katika kiti cha gari, anakufa.

## *Padri Luigi Carrara anauawa*

Padri Luigi Carrara alikuwa kanisani kwa kuungamisha wakristu. Akiona namna gani frera aliuawa, anatoka na sitola "violet" mabegani kwa kukutana na "Colonnel". Abedi anasema:

"Nakubeba mpaka Fizi kwa kukuua pamoja na mapadri wengine".

Padri Luigi alimjibia:

"Kama unapenda kuniua, napenda zaidi kufa hapa pamoja na ndugu yangu".

Ndiyo maneno yake ya mwisho. Padri Luigi hakuongeza neno, hakungoja jibu. Alipiga magoti karibu na maiti ya frera kwa kusali. Risasi moja ilitosha kwa kuvunja kifua cha Padri Carrara Luigi na kumwua. Nyuma ya kuwaua na kukata vipande vya mwili wao, wamulele walitembea katika mji wa Baraka, wakibeba juu ya kibao vipande vile.

## Padri Giovanni Didonè anauawa

Siku ile ile ya 28 Novemba, kiisha kuwaua wandugu 2 wa Baraka, Abedi Masanga anapanda tena Fizi. Katika safari ya km 29, njiani Abedi alipata namna ya kuongeza hasira na hamu ya kuwaua pia Mapadri wa Fizi. Akifika Fizi, alienda kwanza katika "Quartier Général du Général Shabani". Abedi anamwadisia Shabani namna gani aliwaua Mapadri wa Baraka, tena anamwonyesha nia ya kuua pia Mapadri wa Fizi. Général na Colonnel wanaongea kati yao:

> "Kama unaua Mapadri, unapata faida gani? Sasa wale wa Baraka walikufa, namna gani wanaweza kuendelea kuishi wale wa Fizi?"

Mangaribi, labda saa kumi na mbili, gari ya Abedi (mlango uko na tundu, na alama ya damu katika kiti cha mbele) inasimama mbele ya sanamu ya Bikira Maria, karibu na kanisa. Akitoka kwa gari, Abedi, na sauti kubwa anamwita Padri. Padri Giovanni Didonè anatoka nje, haoni hata kama Abedi anamwangalia na bunduki (révolver) mikononi. Risasi inamkamata Giovanni katika panda la uso. Giovanni, bila kulalamika, anaanguka karibu na papayo na anakufa.

## Abbé Albert Joubert anauawa

Padri Albert anatoka kwa nyumba ndogo kwa kuangalia inatukia nini. Aliona uuaji wa Padri Didonè, moyo wake unageuka kuwa kama vile jiwe. Dakika moja ya woga kubwa. Hapo Albert anajaribu kujitupa katika mtelemuko ya mlima mdogo, karibu na nyumba ndogo ya mbao. Hakuna namna: risasi inavunja moyo wake; Albert anaanguka udongoni, katikati ya majani ya kichaka, anakufa. Abedi, na moyo baridi baridi,

bunduki (révolver) mikononi, anapanda katika gari yake na usiku mzima anafanya fujo na ujeuri.
Kesho yake asubui na mapema msermala wa Misioni anakuja kwa kazi; anakuta maiti mawili chini, udongoni; kwa msaada wa rafiki mmoja anazika Mapadri wawili katika shimu iliyokuwa katika kiwandja cha masomo Luundo.





Kanisa Katoliki ya Baraka (1966) na ya Fizi (1962)

Kiisha uuaji, Faccin na Didonè walizikwa nyuma ya nyumba ya Mapadri, itakayokuwa kiisha nyumba ya Masera ya “Saint Joseph de Turin”, na siku hizi “Hopital des Médecins sans Frontières”. Didonè na Joubert walizikwa Fizi katika tundu iliyokuwa tayari kwa maji chafu, katika kiwandja cha masomo Luundo.

Padri Palmiro Cima aligundua maiti ya Carrara na Faccin kwa kuyapeleka, kwa njia ya Kalemie, mpaka Cyangugu (Rwanda) katika nyumba ya Diosezi ya Uvira. Mwaka 1972 maiti ya Carrara na Faccin walirudishwa tena Baraka na walizikwa katika kanisa, nyuma ya altare. Vile vile maiti ya Joubert et Didonè, kutoka Fizi yalizikwa tena katika kanisa ya Baraka.

Siku 23.6.1968, katika maandamano ya shangwe na imani, iliyoongozwa na Askofu Catarzi, maiti ya Joubert na Didonè yanarudishwa katika nafasi ya kifo chao cha sifa, Fizi, mashahidi wa Yesu. Wakristu walitoka pande zote ya Misioni ya Fizi kwa kuwashangilia watumishi wa Mungu waliokufa kwa ajili ya Enjili, wakiimba na furaha na shangwe katika njia za Fizi, mpaka Kanisa, kwenye sasa wanapunzika.

## Kipindi cha 24: Wandugu wetu hawa wanne ni mashahidi wa kweli

Eklezya katolika inataja Wenye heri na Watakatifu wale wakristu waliouawa sababu ya chuki ya imani cha wauaji (odium fidei ex parte persecutoris). Sababu hiyo ni ngambo ya wauaji. Lakini ngambo ya mashahidi kubakia katika nafasi ya hatari ya kufa kwa mapendo ya Mungu na ya wandugu ni ushuhuda wa kifo. Luc de l'Arbre, juu ya mashahidi wa Congo wa wakati huo, anasema hivi:

> "Wote walibakia na moyo mwema katika Misioni yao, japo zoruba ilikuwa tayari, kama vile mashahidi wa Kristu, kwa ajili ya mapendo ya wandugu na wadada. Halafu wapo mashahidi wa kweli wa Enjili, mpaka kufa, mashahidi wa kweli wa Yesu Kristu, mashahidi wa mapendo ya Mungu na ya watu walioaminiwa kwao".

Mashahidi wetu walijua hatari ya kifo, kiisha uuaji wa Lumumba (17.1.61), kiisha uuaji wa 22 Wamisionari "Spiritains" pa Kindu (1.1.61); walijua pia namna gani walifungwa na waliteswa Uvira, muda wa miezi 5, Askofu Catarzi pamoja na Mapadri na Masera. Halafu kwa ajili ya Mashahidi wetu, kifo hakikuwa kitisho cha rafla, ila kinyume wazi wanachokubali na utashi wote, wao wenyewe: kubakia pamoja na wandugu walioaminiwa kwao.

Lakini chuki ya imani ya wauaji (odium fidei ex parte persecutoris) ilikuwa pia alama wazi ya ushuhuda wa damu wa wandugu wetu. Kati ya Wamulele wamoja walikuwa wanafanya "agano na shetani" kwa kuweza kushinda vita na kuua adui, bila kuuawa wenyewe. Wakubwa wamoja wa Wasimba hawakuwa na dini, ila waliadibishwa kuishi bila Mungu, pa Moscou, Péquin, Caire na Cuba.

Padri Pansa aliona katika nyumba ya mkubwa wa Wamulele sanamu ya shetani anayemzarau Yesu Kristu. Pa Baraka Wamule walizoea mchezo wa kupiga masasi kwa sanamu ya Bikira Maria.

## Vittorio Faccin

Frera Vittorio Faccin ni mshahidi wa kweli wa Yesu Kristu. Alijua kama labda atauawa, hakuogopa, hakukimbia, alibakia tu pamoja na kondoo za Mungu, wote ndugu na dada zake.

Frera Vittorio Faccin alibakia tu katika Misioni yake. Kiini cha kuwa misionari ni kubakia pamoja na watu, kama Mchungaji mwema. Kiini cha kuwa Mshahidi wa damu wa Yesu Kristu, ni kubakia pamoja na watu.

Kila Mwenye Heri ao Mtakatifu, kwa njia ya maisha yake na kufa kwake anaandika tena mstari mmoja wa Enjili. Frera Vittorio Faccin alifanana na Yesu Mchungaji mwema:

> "Mchungaji mwema atoa uzima wake kwa ajili ya kondoo.
> Mtu wa mshahara, asiye mchungaji wala mwenyeji wa kondoo,
> akimwona mbwa mwitu anakuja, anawaacha kondoo, anakimbia"
> (Yoane 10, 11-12).

## Luigi Carrara

Padri Luigi Carrara ni mshahidi wa kweli wa Yesu Kristu. Alijua kama labda atauawa, hakuogopa, hakukimbia, alibakia tu pamoja na kondoo za Mungu, wote ndugu na dada zake.

P. Luigi Carrara alibakia tu katika Misioni yake. Kiini cha kuwa misionari ni kubakia pamoja na watu. Kiini cha kuwa Mshahidi wa damu wa Yesu Kristu, ni kubakia pamoja na watu.

Kila Mwenye Heri ao Mtakatifu, kwa njia ya maisha yake na kufa kwake anaandika tena mstari mmoja wa Enjili. P. Luigi Carrara aliandika:

> "Furahini, shangilieni,
> kwani tuzo yenu itakuwa kubwa mbinguni" (Mateo 5, 12).

## Giovanni Didonè

Padri Giovanni Didonè ni mshahidi wa kweli wa Yesu Kristu. Alijua kama labda atauawa, hakuogopa, hakukimbia, alibakia tu pamoja na kondoo za Mungu, wote ndugu na dada zake.

P. Giovanni Didonè alibakia tu katika Misioni yake. Kiini cha kuwa misionari ni kubakia pamoja na watu. Kiini cha kuwa Mshahidi wa damu wa Yesu Kristu, ni kubakia pamoja na watu.

Kila Mwenye Heri ao Mtakatifu, kwa njia ya maisha yake na kufa kwake anaandika tena mstari mmoja wa Enjili. Padri Giovanni Didonè aliandika heri ya nane:

"Heri wenye kuzulumiwa sababu ya unyofu,
kwani Ufalme wa mbingu ni wao" (Mt 5, 10).

## Albert Joubert

Padri mkongomani Albert Joubert, mshahidi wa Yesu Kristu, alikuwa mtu mnyenyekevu na mnyamavu. Mashahidi wetu wengine walisema, waliandika barua kwa wazazi kwa kuonyesha nia yao ya kubakia katika Misioni yao, japo hatari ya kufa. Albert hakusema kitu, hakuandika barua kwa kuonyesha nia yake, ila alitenda: katika kimya na unyenyekevu. Albert alibakia tu katika Misioni yake. Kiini cha kuwa misionari ni kubakia pamoja na watu. Kiini cha kuwa Mshahidi wa damu wa Yesu Kristu, ni kubakia pamoja na watu.

Kila Mwenye Heri ao Mtakatifu, kwa njia ya maisha yake na kufa kwake anaandika tena mstari mmoja wa Enjili. Padri Mkongomani Albert Joubert aliandika hivi:

"Nanyi mtachukiwa na wote kwa ajili ya jina langu,
lakini atakayekaa imara mpaka mwisho, ndiye atakayeokoka"
(Mateo 10, 22).

# Yaliyomo

SEHEMU YA KWANZA: hali ya Congo mwaka 1964 .................. 2
Kipindi cha 1: Congo katika zoruba kiisha uhuru..................... 2
Kipindi cha 2: Zoruba katika diosezi ya Uvira na Bukavu ...... 4
Kipindi cha 3: Mashahidi wa Kristu wakati wa zoruba ........... 9
Kipindi cha 4: Historia ya Mashahidi wengine....................... 11
Kipindi cha 5: Wenye heri Anwarite Clementine Nengapeta na Francesco Spoto ............................................................... 20
SEHEMU YA PILI: FRERA VITTORIO FACCIN ....................... 23
Kipindi cha 6: Frera Vittorio Faccin ni nani? ......................... 24
Kipindi cha 7: Faccin anajitayarisha kuwa Misionari............ 26
Kipindi cha 8: Vittorio, Misionari katika Congo .................... 28
Kipindi cha 9: Zoruba inakaribia.......................................... 32
SEHEMU YA TATU: PADRI LUIGI CARRARA........................ 34
Kipindi cha 10: Luigi Giuseppe Carrara ni nani? .................. 35
Kipindi cha 11: Luigi anajitayarisha kwa kuwa Misionari..... 37
Kipindi cha 12: Luigi anatumwa kuwa Misionari.................. 39
Kipindi cha 13: Luigi anafika Congo ...................................... 40
Kipindi cha 14: Zoruba inakaribia ......................................... 45
SEHEMU YA NNE: PADRI GIOVANNI DIDONÈ..................... 46
Kipindi cha 15: Giovanni Didonè ni nani?.............................. 47
Kipindi cha 16: Matayarisho kwa kuwa Misionari ................ 49
Kipindi cha 17: Padri Giovanni anatumwa Congo................. 51
Kipindi cha 18: Zoruba kiisha uhuru..................................... 52
SEHEMU YA TANO: ABBÉ ALBERT JOUBERT ...................... 53

Kipindi cha 19: Jamaa ya Abbé Albert .................................... 54
Kipindi cha 20: Albert katika Seminario ................................ 56
Kipindi cha 21: Utumishi wa Abbé Albert ............................... 58
SEHEMU YA SITA: KIFO CHA MASHAHIDI WETU............... 61
Kipindi cha 22: Wandugu wetu wanne wanakufa kwa ajili ya Yesu........................................................................................ 62
Kipindi cha 23: Mazishi ya mashahidi wetu ........................... 65
Kipindi cha 24: Wandugu wetu hawa wanne ni mashahidi wa kweli......................................................................................... 66
Mwisho ........................................................................................ 67



Katika kitabu hicho, padri Mario Sciamanna, Missionario Xaveriano, alitimiza maagizo ya Mt. Papa Paulo ya sita, alipomwambia Mgr Catarzi, askofu wa Uvira, ya kwamba wakristu wanaitwa kuandika historia ya Faccin, Carrara, Didonè na Joubert kwani ni mashaidi wa imani wa Congo.
Sciamanna anawaheshimu waliouawa pa Baraka na Fizi, tarehe 28 novemba 1964 na kutusaidia kuwafahamu vizuri zaidi.



Papa Paulo VI pamoja na Catarzi Danilo, askofu wa Uvira
(Roma 27.09.1978)